# Uraia na Maadili

## Kitabu cha Mwanafunzi

### Darasa la Nne



Taasisi ya Elimu Tanzania

*Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Uraia na Maadili

## Kitabu cha Mwanafunzi

## Darasa la Nne



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 559

Jina la Chapisho: Uraia na Maadili Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9987-09-324-3

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 12 Julai, 2021 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Darasa la Nne katika ngazi ya elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa Mwaka 2016.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

FOR ONLINE USE ONLY

Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2018

Toleo la Kwanza 2018

Toleo la Pili 2021

ISBN: 978 – 9987 – 09 – 324 – 3

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P 35094
Dar-es-Salaam, Tanzania

Simu: +255735041170/+255735041168
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

FOR ONLINE USE ONLY

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote bila idhini ya maandishi ya Taasisi ya Elimu Tanzania.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Yaliyomo

**Shukurani**..........v

**Utangulizi**..........vi

**Sura ya Kwanza**
Kujipenda na kuwapenda watu wengine..........1

**Sura ya Pili**
Kuipenda shule yetu..........16

**Sura ya Tatu**
Kuipenda nchi yetu..........28

**Sura ya Nne**
Demokrasia..........43

**Sura ya Tano**
Kujijali na kuwajali watu wengine..........54

**Sura ya Sita**
Kuwajibika na kulinda rasilimali..........71

**Sura ya Saba**
Kutii sheria na kanuni..........83

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Sura ya Nane**
Kuwa mvumilivu........................................................................94

**Sura ya Tisa**
Kufikia malengo.................................................................... 102

**Sura ya Kumi**
Kujifunza mambo kiyakinifu........ .......................................116

**Sura ya Kumi na Moja**
Kuishi na watu wa asili tofauti........ ....................................124

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


## Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi wa kitabu hiki.

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wote walioshiriki kutayarisha kitabu hiki wakiwemo wachapaji, wasanifu, wahariri, wachoraji na wapiga chapa. Pia, inatoa shukurani kwa shule zote zilizoshiriki katika ujaribishaji wa maudhui ya kitabu hiki.

Aidha, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Shirika la "Global Partnership for Education (GPE)" kupitia Mradi wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) uitwao "Literacy and Numeracy Education Support (LANES)" kwa ufadhili wao uliofanikisha kazi ya kutayarisha na kuchapa kitabu hiki.

Mwisho, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kusimamia kwa karibu zoezi zima la uandishi wa kitabu hiki.

**Dkt. Aneth A. Komba**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Taasisi ya Elimu Tanzania**


FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Utangulizi

Kitabu hiki kimeandaliwa kulingana na muhtasari wa Uraia na Maadili wa mwaka 2016 ambao unazingatia ujenzi wa umahiri. Ni mwendelezo wa Kitabu cha Uraia na Maadili Darasa la Tatu.

Kitabu hiki kina sura kumi na moja na kila sura imeundwa na vipengele kadhaa. Sura hizo zimejengwa kwa maudhui yaliyowasilishwa kwa visa, habari, mazungumzo, na majigambo. Pia, maudhui mengine yamewasilishwa kwa ngonjera, nyimbo na mashairi. Kila sura ina mazoezi na kazi za kufanya. Pia, ufafanuzi wa msamiati umetolewa mwishoni mwa kila sura.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kwanza

## Kujipenda na kuwapenda watu wengine

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza kubaini matendo ya kujipenda na kuwapenda watu wengine katika jamii. Pia, utajifunza kubaini matendo yanayohatarisha usalama wa watoto na wanajamii. Aidha, utajifunza namna na umuhimu wa kuzingatia maelekezo na miongozo sahihi unayopewa nyumbani na shuleni. Umahiri utakaoupata katika sura hii utakuwezesha kutambua wajibu wako wa kuheshimu na kuwapenda watu wote katika jamii yako.*

### Matendo yanayoonesha upendo katika jamii

Kuna matendo mengi yanayoonesha kujipenda na kuwapenda watu wengine katika jamii. Baadhi ya matendo hayo ni kujiheshimu na kuwaheshimu watu wengine, kujijali na kuwajali watu wengine pamoja na kujikinga na kuwakinga watu wengine dhidi ya mambo yanayoweza kuwadhuru. Pia, kuwasaidia walemavu, wagonjwa na wazee.

### Matendo yanayoonesha upendo kwa familia

Katika familia kuna watu mbalimbali kama vile baba, mama, dada na kaka. Pia wapo babu na bibi, mama wadogo na wakubwa, wajomba, binamu na wengine. Sisi wanafamilia tunapaswa kujipenda na kuwapenda wanafamilia wenzetu.

Katika familia, watu wanapaswa kuishi kwa upendo na mshikamano. Wanafamilia wanapaswa kula pamoja, kufanya kazi pamoja na kusaidiana katika shida na raha.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Katika mila na desturi ni mwiko kumchukia ndugu yako wa damu.Vipo vitendo mbalimbali vinavyofanywa na wanafamilia kuonesha upendo. Kwa mfano kusaidiana kwenye shida mbalimbali kama vile njaa, maradhi na mengineyo. Pia, tunatakiwa kuwa mstari wa mbele kuwakosoa ndugu zetu wanapokosea ili waweze kujirudi katika mwenendo stahiki.

Je, ni matendo gani ya upendo ungependa utendewe na wanafamilia? Ni matendo gani ya upendo unayowatendea wanafamilia?

Miongoni mwa matendo yenye kuonesha upendo katika familia ni kushiriki katika shughuli za nyumbani. Je, ni shughuli gani unazifanya ukiwa nyumbani?

*Soma mazungumzo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Mama Sikitu:** Habari za nyumbani rafiki yangu.

**Mama Furaha:** Nzuri tu, vipi mwanao Sikitu hajambo?

**Mama Sikitu:** Hajambo! Furaha anaendeleaje?

**Mama Furaha:** Furaha anaendelea vizuri na ananisaidia sana katika shughuli za nyumbani. Kila alfajiri anapoamka anaosha vyombo na kufagia uwanja. Pia huchota maji ndipo aende shuleni. Akirudi jioni humwagilia bustani ya mboga na kunisaidia kuandaa chakula.

**Mama Sikitu:** Heri yako mwenzangu, binti yangu Sikitu ni mvivu sana. Hafanyi kazi yoyote nyumbani, si kufagia, wala kuosha vyombo. Hata nguo zake namfulia na kumpigia pasi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mama Furaha:** Pole mwenzangu! Inawezekana unamdekeza sana Sikitu.

**Mama Sikitu:** Hapana rafiki yangu. Nimejitahidi kumwelekeza hadi nimechoka. Sikitu hanielewi hata kidogo.

**Mama Furaha:** Usikate tamaa. Jaribu kukaa naye na kumshauri. Mfanye kuwa rafiki yako wa karibu. Mueleze faida za kushiriki katika kazi za nyumbani. Muelekeze kwa upendo na si kwa kumfokea, taratibu atabadilika tu.

### Zoezi la 1

1. Taja matendo matatu yanayoonesha kujipenda mbali na yaliyoelezwa katika kitabu.
2. Taja matendo matatu yanayoonesha kuwapenda watu wengine katika jamii.
3. Mama Sikitu anavutiwa na matendo gani anayoyafanya Furaha?
4. Je, ni matendo yapi mengine ya upendo yanayofaa kuigwa na wanafamilia?
5. Je, ni mambo gani ya upendo unayopenda kufanyiwa na familia yako?
6. Kama wewe ungekuwa rafiki yake Sikitu ungefanya nini kumsaidia?

### Kazi ya kufanya

Andika kwenye daftari lako matendo mengine matano yanayoonesha upendo katika familia. Kisha kusanya kazi hiyo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kuwahudumia wanafamilia wenye mahitaji maalumu

Familia zetu hujengwa na watu wenye mahitaji mbalimbali. Watu hao ni kama watoto wadogo, walemavu, wazee, wagonjwa na wajawazito. Ni vyema kujifunza mahitaji yao ili kuwasaidia.

*Hebu tafakari matendo yafuatayo:*

1. Mtoto anapika chakula cha mama yake ambaye ni mgonjwa.
2. Kaka anampeleka mdogo wake hospitali.
3. Dada anafua nguo za mdogo wake anayeumwa.
4. Watoto wanamnyanyua baba yao mlemavu na kumsaidia kukaa kwenye baiskeli.
5. Mtoto anampelekea bibi maji ya kunywa.

Je, umejifunza nini kupitia matendo haya?

*Soma kisa kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Bwana na Bibi Sheuta wanaishi kijiji cha Soni, wilaya ya Lushoto. Wana watoto watatu; Bakari, Sharifa na Amina. Bakari anasoma darasa la pili. Amina anasoma darasa la tatu, na Sharifa anasoma darasa la nne. Bakari ni mlemavu wa miguu. Kila siku asubuhi Sharifa na Amina humsaidia mdogo wao kuvuka barabara wanapokwenda shuleni. Hufanya hivyo tena wanaporudi kutoka shuleni. Pia, familia hii huishi na bibi Saufa ambaye ni mzee sana, na macho yake hayaoni vizuri.

Sharifa humshika mkono bibi Saufa na kumsindikiza anapoenda bafuni kuoga. Pia humwandalia chakula na maji ya kunywa. Amina humsaidia mama yake kupika chakula na kufua nguo za wanafamilia. Vilevile, humsaidia Bakari kujenga stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 2**

1. Je, ni tabia zipi zinazofaa kutokana na kisa hiki?
2. Je, wewe unafanya matendo yapi kuwahudumia wanafamilia wenye mahitaji maalumu?
3. Utamshauri nini mwenzako asiyependa kuwahudumia wanafamilia wenye mahitaji maalumu?

## Kuwasaidia wanafamilia wanapopatwa na matatizo

Ni muhimu kuwasaidia watu wengine katika familia ili kutatua matatizo yao. Utafanya nini iwapo;

1. Mdogo wako amejikata na wembe kwenye kidole na damu inamtoka?
2. Mama au baba yako ameugua ghafla mkiwa peke yenu nyumbani?
3. Mdogo wako amejisaidia kwenye kaptula?
4. Dada au kaka yako amepoteza daftari lake?

*Soma ngonjera ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Bahati:** Habarini ndugu zangu,
Ujumbe nawaletea,
Ndugu kusaidiana,
Na siyo tu kufanana.

**Salama:** Mbona unanichanganya,
Wataka kunidanganya,
Msaada huo ni upi?
Mbona sikuelewi?

**Bahati:** Wazazi kuwauguza,

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Wanapokuwa wagonjwa,
Ndugu kuwahudumia,
Wanapokuwa na shida.

**Zawadi:** Faraja tunapeana,
Panapokuwa na tabu,
Suluhisha ugomvi,
Pale unapotokea.

**Salama:** Sasa nimewaelewa,
Elimu nimeipata,
Familia tuijali,
Ikiwa na matatizo.

**Zoezi la 3**

1. Unapata ujumbe gani kutokana na ngonjera hii?
2. Ni kwa namna gani unaweza kuwasaidia wanafamilia wenzako wanapokuwa na matatizo?
3. Kuna umuhimu gani mwingine ambao haukutajwa katika ngonjera hii unaotokana na kuwasaidia wanafamilia wanaopatwa na matatizo?

**Kazi ya kufanya**

Orodhesha kwenye daftari lako matendo matano yanayofaa kuwatendea wanafamilia.

## Kusaidia kulea wadogo zako

Katika sehemu hii utajifunza matendo na umuhimu wa kuwajali na kuwalea wadogo zako. Ukifanya hivyo utawasaidia wakue vyema.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Angalia picha zifuatazo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

1.



2.



3.



**Kielelezo namba 1:** *Matendo ya kusaidia kulea wadogo zako*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

1. Ni matendo yapi yanayoonekana kwenye picha ya kwanza hadi ya tatu?
2. Je, ni matendo yapi kati ya hayo unayafanya ukiwa nyumbani?
3. Ni matendo yapi tofauti na yaliyopo kwenye picha unayafanya ukiwa nyumbani?

## Kazi ya kufanya

Zungumza na wazazi, walezi au ndugu zako kuhusu matendo unayotakiwa kufanya kuwalea wadogo zako. Andika matendo hayo nyuma ya daftari lako. Chora jedwali linaloonesha matendo ya kulea wadogo zako. Kisha onesha kwa idadi jinsi ulivyotenda matendo hayo kwa wiki moja. Zingatia mfano ufuatao:

Mfano wa jedwali

| Siku za wiki | Matendo | Idadi ya matendo |
|---|---|---|
| Jumatatu | Kumuogesha Mtoto | 2 |

Baada ya wiki moja, muoneshe jedwali lako mwalimu wa Uraia na Maadili.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Matendo yanayohatarisha usalama katika jamii

Ni jukumu letu kuhakikisha kuwa familia na wanajamii wanakuwa salama wakati wote. Hii ina maana kuwa, ni muhimu kuyatambua na kuyaepuka matendo yanayohatarisha usalama katika jamii. Matendo hayo ni pamoja na kupuuza sheria za barabarani, kushiriki ajira za utotoni na kujiunga na makundi yanayotumia vilevi kama vile pombe, bangi na vinginevyo.

**Kazi ya kufanya**

Angalia matendo yanayohatarisha usalama wa mtoto yanayofanyika katika maeneo yanayokuzunguka. Andika matendo hayo kwenye daftari lako.

## Madhara ya matendo yanayohatarisha usalama wa watoto

Bila shaka unatambua kuwa matendo yanayohatarisha usalama wa watoto yana madhara mbalimbali.

*Soma mazungumzo haya, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Babu:** Hamjambo wajukuu zangu?

**Wajukuu:** Hatujambo! Shikamoo babu.

**Babu:** Marahaba! Leo nataka tujadili kuhusu vitendo vinavyohatarisha usalama wa watoto. Je, kuna anayeweza kutaja moja ya vitendo hivyo?

**Samata:** Kushiriki katika ajira za utotoni.

**Babu:** Vizuri Samata. Je, umewahi kuona watoto wakishiriki kwenye ajira za utotoni?

**Selina:** Ndiyo babu. Nimewaona watoto wakishiriki ajira za utotoni, kwa mfano; kubeba mizigo mizito, kuponda kokoto za ujenzi, na kuchimba madini.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Babu:** Aahh! Hii ni hatari sana kwa afya zao. Ni jambo gani jingine linaweza kuhatarisha maisha ya mtoto?

**Fatuma:** Kupuuza sheria za barabarani kunakosababisha ajali kwa wanafunzi.

**Babu:** Ndiyo mjukuu wangu Fatuma, umejibu vizuri sana. Baadhi ya madereva hupuuza sheria za barabarani wanapoendesha magari na pikipiki. Hivyo wanaweza kuwagonga watoto na kuwasababishia vifo au ulemavu wa kudumu.

**Yakobo:** Mimi nadhani pia, watoto wanaweza kujihusisha na makundi hatarishi.

**Babu:** Ndiyo Yakobo. Unaweza kueleza zaidi kuhusu makundi hatarishi?

**Yakobo:** Haya hujumuisha makundi ya watumiaji wa vilevi kama pombe au dawa za kulevya. Pia, watoto huweza kushiriki ngono wakiwa na umri mdogo.

**Babu:** Nani anaweza kutueleza madhara ya kushiriki ngono katika umri mdogo?

**Upendo:** Watoto wanaweza kupata mimba za utotoni na kukatisha masomo yao. Pia, wanaweza kupata maambukizi ya magonjwa ya zinaa kama vile UKIMWI na Kaswende.

**Babu:** Vitendo hivi ni hatarishi kwa usalama wa watoto na raia wengine. Wajukuu zangu ninawaasa muwe na tabia njema. Msihatarishe usalama wa maisha yenu.

**Samata:** Asante babu kwa nasaha zako.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5

1. Je, ni vitendo gani hatarishi kwa usalama wa watoto?
2. Ni madhara yapi yanayotokana na vitendo vinavyohatarisha usalama wa watoto?
3. Je, ni vitendo gani kati ya vilivyotajwa kwenye mazungumzo ni hatarishi zaidi?
4. Unafikiri ni ushauri gani zaidi babu angetoa kuhusu ulinzi na usalama?
5. Utawasaidiaje wenzako kuepuka vitendo hatarishi?

## Zoezi la 6

Andika **ndiyo** mbele ya sentensi sahihi au **hapana** mbele ya sentensi isiyo sahihi.

1. Ni vyema kuwatendea wengine vitendo usivyopenda kutendewa ____________.
2. Wanafunzi wanapaswa kuzingatia maelekezo wanayopewa na walimu tu ______________.
3. Njia bora ya kumfundisha mwanafunzi mvivu ni kumchapa ____________.
4. Watoto wadogo, wagonjwa na walemavu wanahitaji kuhudumiwa ______________.
5. Wanafamilia wanapaswa kusaidiana wakati wa matatizo tu _____________.
6. Kutumia vilevi na kushiriki ngono katika umri mdogo ni vitendo hatarishi _____________.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Matendo yanayoharibu upendo katika jamii

*Tafakari matendo yafuatayo:*

1. Mwanafunzi anamrushia jiwe mwenzake.
2. Mwanafunzi anamsengenya rafiki yake.
3. Mwanafunzi anamtukana mwenzake.
4. Mtoto anasema uongo ili apewe fedha na mzazi au mlezi wake.

Bila shaka umewahi kuona watu wakitenda matendo yanayoharibu upendo katika jamii. Matendo hayo ni kama vile ugomvi, kusengenya na kutukana. Pia matendo mengine ni uchoyo, wizi na udanganyifu.

*Soma kisa kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Shukuru na Sekela ni wanafunzi wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Jitegemee. Kila asubuhi Sekela hupewa fedha kwa ajili ya nauli na matumizi mengine. Licha ya kupewa fedha za kutosha, Sekela huwadanganya wazazi wake ili apewe fedha zaidi. Akiwa shuleni, hununua sharubati na vitumbua na kula peke yake. Siku moja Shukuru alipoteza kalamu yake, akamuomba Sekela amsaidie. Sekela alikuwa na kalamu mbili, lakini alikataa kumsaidia Shukuru. Wakati wa mapumziko, Shukuru hupenda kucheza na marafiki zake. Wote huacha mifuko ya madaftari yao darasani. Sekela hubaki darasani kwa sababu hapendi kucheza na wenzake. Siku moja wakati wa mapumziko, Shukuru na wenzake walikuwa wakicheza nje. Sekela alichungulia dirishani na kuona kuwa hakuna mtu anayemuona. Akafungua mfuko wa Shukuru na kuiba rula. Baada ya mapumziko, Shukuru alirudi darasani akashangaa kuona mfuko wake ukiwa wazi. Alipoangalia ndani hakuiona rula yake. Alikimbia ofisini na kumtaarifu mwalimu wa darasa kuhusu kupotea kwa rula yake.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mwalimu alikuja darasani na kuwakagua wanafunzi katika mifuko yao. Ahhh! Rula ilikuwa imefichwa ndani ya mfuko wa Sekela. Mwalimu alimuonya Sekela aache tabia ya wizi.

Halafu akasisitiza kwamba, mwanafunzi inakupasa utambue kuwa si vyema kuwatendea wengine matendo usivyopenda kutendewa. Hivyo basi, yakupasa kutenda matendo yanayofaa kila wakati katika maisha yako.

**Zoezi la 7**

1. Je, ni matendo yapi yasiyofaa kumtendea mtu yaliyo katika kisa hiki?
2. Una maoni gani kuhusu matendo ya Sekela?
3. Utafanya nini kumsaidia mwenzako kuepuka tabia kama ya Sekela?
4. Ni matendo yapi mengine yasiyofaa kumtendea mtu zaidi ya haya yaliyooneshwa kwenye kisa ulichosoma?

**Kazi ya kufanya**

Zungumza na wazazi au walezi au wanafunzi wenzako kuhusu umuhimu wa kuepuka matendo yasiyofaa kumtendea mtu. Andika mazungumzo hayo kwenye daftari lako.

## Kuzingatia maelekezo ya walimu, wazazi na walezi

Je, umewahi kupewa maelekezo na mzazi, mlezi au mwalimu?

*Soma kisa kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Adila ni mtoto wa Mzee Shokolo. Anasoma Shule ya Msingi

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kirore. Mzee Shokolo humuelekeza Adila kazi za nyumbani. Mara nyingi maelekezo hufanyika kabla ya kwenda shule na baada ya kurudi nyumbani. Kazi hizo ni kufagia uwanja, kuosha vyombo na kuteka maji. Kazi nyingine ni kumwagilia bustani ya mboga na maua. Pia humuelekeza kufua na kunyoosha nguo zake na kufanya kazi alizopewa shuleni.

Kila siku asubuhi, Adila huosha vyombo na hufagia uwanja. Aidha, Adila hufika shuleni mapema, hufanya usafi kisha humwagilia maua. Wakati wa jioni, Adila hurejea nyumbani na humwagilia bustani. Walimu, wazazi na jamii hufurahishwa sana na tabia ya usikivu wa Adila. Kwa sababu hiyo, Adila hupokea zawadi nyingi kutoka kwa wazazi, walezi, walimu na wanajamii.

## Zoezi la 8

1. Je, ni matendo yapi ya Adila yanayofaa kuigwa?
2. Je, ni maelekezo gani Adila hupewa nyumbani na shuleni?
3. Kwa nini ni muhimu kuzingatia maelekezo sahihi unayopewa?
4. Utamsaidiaje mwenzako asiyependa kuzingatia maelekezo ya walimu, na wazazi au walezi?
5. Orodhesha faida tatu za kufuata maelekezo unayopewa na wazazi, walezi au walimu.

## Kazi ya kufanya

Andika orodha ya shughuli unazofanya kila siku. Bainisha shughuli unazofanya kwa kufuata maelekezo ya mzazi, mlezi, au mwalimu. Bainisha shughuli unazofanya bila kufuata maelekezo ya mzazi, mlezi au mwalimu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Ajira | kazi ya kulipwa mshahara au kujiajiri |
| Dhamira | jambo analokusudia mtu kufanya |
| Hatarishi | yenye kuleta madhara |
| Nasaha | maneno mazuri yanayotolewa kushauri jambo |
| Sharubati | kinywaji kinachotengenezwa kwa maji ya matunda |
| Wanajamii | ni jumuiya ya watu wanaoishi katika eneo fulani |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Pili

## Kuipenda shule yetu

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza kutunza mazingira ya shule na muundo wa uongozi wa shule. Vilevile, utajifunza sheria na kanuni za shule, na shughuli zenye kuiletea shule sifa nzuri. Umahiri utakaoupata katika sura hii utakuwezesha kutii sheria na kanuni zilizowekwa katika jamii.*

### Muundo wa uongozi wa shule

Ni vyema utambue kuwa viongozi wa shule wana mchango mkubwa katika ujifunzaji shuleni. Viongozi hao wanasaidia kuboresha nidhamu yenu, maendeleo ya kitaaluma na mazingira ya shule yenu. Viongozi wa shule yako hutofautiana kwa majukumu mbalimbali. Mpangilio wa viongozi katika nafasi na majukumu yao huitwa muundo wa uongozi wa shule.

Je, unawafahamu viongozi wa shule yako? Unaufahamu muundo wa uongozi katika shule yako? Je, viongozi wa shule yako wana majukumu yapi?

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Shule ya Msingi Maendeleo ni moja ya shule kongwe nchini. *Je, ungependa kufahamu uongozi wa shule hii?* Uongozi wa shule hii unaundwa na kamati ya shule, mwalimu mkuu, mwalimu mkuu msaidizi, mwalimu wa taaluma, mwalimu wa nidhamu, walimu, na viranja.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Muundo wa Uongozi wa Shule




**Kielelezo namba 1:** *Muundo wa uongozi wa shule za msingi*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 1**

1. Je, ni viongozi gani wa shule wanaotajwa kwenye habari hii?
2. Nini faida ya kuwa na viranja shuleni?
3. Je, unapata faida gani kwa kuwafahamu viongozi wa shule yako?

**Kazi ya kufanya**

Jadiliana na mwalimu wako wa somo kuhusu majukumu ya Kamati ya shule, Mkuu wa shule, Mwalimu Mkuu Msaidizi, Mwalimu wa Taaluma, na Mwalimu wa Nidhamu.

FOR ONLINE USE ONLY

## Majukumu ya viranja wa shule

Je, ni yapi majukumu ya viranja wa shule?

*Soma majigambo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Kiranja wa usafi**: Mimi nina majukumu mazito, shule inavutia na kupendeza.

**Kiranja wa taaluma**: Wapi wewe! Mimi majukumu yangu ni zaidi ya majukumu yako. Usimamizi wangu ndio unaifanya shule ijulikane kwa ufaulu wa wanafunzi wengi.

**Kiranja wa nidhamu**: Wote mnajidanganya. Hivi mazingira mazuri na ufaulu mkubwa vinapatikanaje bila ya nidhamu nzuri? Mimi jukumu langu ndilo kubwa zaidi.

**Kiranja wa usafi**: Kusimamia usafi wa shule yakiwemo maeneo ya nje na vyoo ni kazi ndogo eeh!

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kiranja wa nidhamu:** Afadhali wewe. Mimi nasimamia wanafunzi kuwahi shuleni. Pia, nahakikisha wanavaa sare za shule zinazotakiwa. Vilevile, wanaingia darasani na kuonesha tabia njema muda wote.

**Kiranja wa taaluma:** Taaluma ndiyo kila kitu. Mimi nasimamia maendeleo ya taaluma ya wanafunzi. Pia, nafuatilia ufundishaji na ujifunzaji darasani na ufaulu katika masomo. Vilevile, natoa ushauri kwa uongozi wa shule kuhusu namna ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

**Kiranja mkuu:** Jamani! Majukumu yenu ni muhimu katika kuiendeleza shule yetu. Nawapongeza nyote kwa usimamizi mzuri unaofanya shule yetu ipate sifa nzuri. Ninayo furaha kuwa msimamizi wenu katika majukumu yote.

**Zoezi la 2**

1. Je, ni kiranja gani mwenye jukumu la kusimamia usafi wa mazingira shuleni?
2. Taja kazi ya kiranja wa darasa.
3. Je, wewe ungependa kuwa kiranja unayesimamia majukumu gani?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kuzingatia sheria na kanuni za shule

Ni wajibu wa kila mwanafunzi kuzingatia sheria na kanuni za shule anaposoma. Je, shuleni kwako kuna sheria na kanuni za shule?

*Hebu tafakari matendo yafuatayo:*

1. Mwanafunzi amegongwa na pikipiki akiwa amevaa shati lisilokuwa na nembo ya shule.
2. Mwanafunzi anazingatia muda wa kufika na kuondoka shuleni.
3. Mwanafunzi hakufanya mitihani kwa sababu ya tabia yake ya utoro.

*Soma kisa kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Shule ya Msingi Amani husifiwa kwa kuwa na wanafunzi wenye nidhamu. Wanafunzi wake wanazingatia sheria na kanuni za shule. Sheria hizo ni kuwahi shuleni, kuhudhuria vipindi vyote, na kuvaa sare zenye nembo ya shule.

Wanafunzi wote hufika shuleni saa moja asubuhi wakiwa wamevalia sare safi za shule. Baada ya paredi vipindi vya masomo huanza rasmi. Vipindi hivyo huanza saa mbili asubuhi hadi saa saba na dakika arobaini mchana.

Mnyate na Asifiwe ni wanafunzi wa darasa la nne katika shule hii. Wanafunzi hawa walikuwa na tabia ya kutoroka shuleni muda wa vipindi. Mara kwa mara mwalimu wa darasa aliwaadhibu na kuwashauri waache utoro lakini hawakuzingatia. Siku moja gari la matangazo lilipita karibu na shule yao. Mnyate na Asifiwe walikuwa makini kusikiliza matangazo hayo. Unadhani

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ni kwa nini walionesha umakini? Wao walikuwa na tabia ya kutoroka shuleni na kwenda kucheza muziki. Tangazo la siku hiyo lilikuwa ni la uzinduzi wa bendi ya muziki. Uzinduzi huo ulikuwa unafanyika mchana wa siku hiyo. Mnyate na Asifiwe walitoroka kwa kuruka ukuta. Kundi kubwa la watu lilihudhuria uzinduzi huo. Mnyate na Asifiwe walisukumwa katikati ya kundi hilo. Walikanyagwa na kupoteza fahamu. Kwa kuwa sare zao za shule zilikuwa hazina nembo ilikuwa ni vigumu kuitambua shule wanayotoka. Hivyo watu wema waliwaweka kando ya barabara na kuwapa huduma ya kwanza.

Punde mwalimu Masumbuko alipita akaona mkusanyiko wa watu. Alisogea karibu ili kujua kilichokuwa kimetokea. Alielezwa kuwa wanafunzi wawili walikanyagwa kwenye uzinduzi wa bendi ya muziki. Mwalimu aliuliza, “Je, wanafunzi hao mmeshawatambua?”. “Bado kwa kuwa sare zao hazina nembo ya shule”, alijibu mmoja wa watu hao. Basi mwalimu Masumbuko alisogea pale walipo wanafunzi wale. “Aaah jamani! Hawa ni wanafunzi wangu”, alisema. Muda huohuo alimpigia simu mwalimu mkuu. Mwalimu mkuu aliagiza wanafunzi wenzao waende kuwabeba na kuwaleta shuleni. Mnyate na Asifiwe walikuwa wameshapata fahamu.

**Zoezi la 3**

1. Ni sheria zipi za shule zilizovunjwa na Mnyate na Asifiwe?
2. Je, utawasaidiaje wanafunzi wenye tabia kama hizi shuleni kwako?
3. Ni athari zipi zinazoweza kumpata mwanafunzi asiyezingatia sheria na kanuni za shule?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Angalia matendo ya kuvunja sheria za shule darasani kwako. Orodhesha kwenye daftari lako matendo yaliyojitokeza mara nyingi.

**Zoezi la 4**

Oanisha maneno ya **kifungu A** na yale ya **kifungu B** ili kupata maana sahihi.

| Kifungu A | Kifungu B |
|---|---|
| 1. Uongozi wa shule | (a) Msimamizi mkuu wa majukumu ya viranja |
| 2. Kiranja Mkuu | (b) Kuwahi shuleni, kuhudhuria vipindi vyote na kuvaa sare zenye nembo ya shule |
| 3. Sheria za shule | (c) Zawadi anayopewa mshindi inayovaliwa shingoni |
| 4. Medali | (d) Kamati ya shule, mwalimu mkuu na mwalimu wa taaluma |
| 5. Sifa nzuri za shule | (e) Kiranja wa taaluma |
| | (f) Wingi wa wanafunzi na walimu |
| | (g) mwalimu mkuu, diwani na viranja |
| | (h) Vikombe |
| | (i) Kufanya vizuri katika taaluma, michezo na nidhamu |

## Kushiriki shughuli zenye kuiletea shule sifa nzuri

Ni vyema ukatambua kuwa kila mwanafunzi ana jukumu la kushiriki katika shughuli mbalimbali. Shughuli hizo ziwe zenye kuiletea shule yake sifa nzuri.

Ni mambo gani yanayoifanya shule yako isifike vizuri kuliko shule za jirani? Je, wewe unashiriki vipi kuiletea sifa shule

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Angalia picha zifuatazo:*

1.




2.




FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3.




4.




**Kilelezo namba 2:** *Matendo ya kuiletea shule sifa nzuri*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 5**

1. Je, ni matendo gani yanaonekana katika picha?
2. Umejifunza nini kutokana na matendo katika picha?
3. Ni matendo gani zaidi ya hayo yanayoweza kuiletea shule yako sifa nzuri?
4. Utatenda matendo gani ili kuiletea shule yako sifa nzuri?

Soma ngonjera ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.

*Hodi hodi twaingia, tunene tuliyonayo,*
*Elimu mliyopata, muitumie maishani,*
*Uhodari mloonesha, shule inajivunia,*
*Sio tu kwenye masomo, tamaduni na michezo,*
*Hamasa tumeipata, mfano tutatumia,*
*Kuletea shule sifa, hiyo ni dhamira yetu.*

*Mmeitangaza shule, hakuna asiyejua,*
*Zawadi mlizopata, shule inajivunia,*
*Nasi pia tutaenzi, sifa shule kujengea,*
*Ufaulu kuongeza, medali kushindania,*
*Hakika hatutashindwa, mikakati twaiweka,*
*Kuletea shule sifa, hiyo ni dhamira yetu.*

*Endelezeni vipaji, dua tunawaombea,*
*Nchi yawategemea, mkae mkitambua,*
*Mmetuonesha njia, nasi tunaipitia,*
*Epukeni na maovu, msije kuangamia,*
*Mafanikio mpate, Taifa lifaidike,*
*Kuletea shule sifa, hiyo ni dhamira yetu.*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 6

1. Unapata ujumbe gani kutokana na ngonjera hii?
2. Ni matendo gani yaliyomo kwenye ngonjera hii yanaweza kuiletea shule sifa nzuri?
3. Je, ni mambo gani mengine yanayoweza kuiletea shule yako sifa nzuri?

## Kazi ya kufanya

Zungumza na marafiki, walezi au wazazi kuhusu mambo waliyoyafanya kuziletea shule zao sifa nzuri. Taja shughuli ambazo hujawahi kuzifanya ili kuiletea shule yako sifa nzuri.

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 7

1. Andika **ndiyo** kwa sentensi sahihi au **hapana** kwa sentensi isiyo sahihi katika sentensi zifuatazo:
   (a) Kushirikiana na wanafunzi wenzetu huweza kuiletea shule sifa nzuri ___________.
   (b) Kusimamia nidhamu ya wanafunzi siyo jukumu la viranja wa shule_____________.
   (c) Utoro wa mwanafunzi huchangia kufeli mitihani ______.
   (d) Jukumu la kuiletea shule sifa nzuri siyo la wanafunzi bali ni la walimu tu _______.
   (e) Tabia njema za wanafunzi ni baadhi ya mambo yanayo iletea shule sifa nzuri _______.
2. Andika habari fupi ukieleza utakavyomhamasisha rafiki yako kushiriki kwenye shughuli zitakazoiletea shule sifa nzuri.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Msamiati**

| | |
|---|---|
| **Athari** | matokeo mazuri au mabaya yampatayo mtu au kitu baada ya kupitia hatua fulani |
| **Katibu** | mwandishi wa taarifa za vikao |
| **Kuenzi** | kuonesha thamani ya jambo zuri lililokwishafanyika |
| **Malezi** | mwongozo mwema anaopewa mtu katika maisha |
| **Medali** | zawadi anayopewa mshindi inayovaliwa shingoni iliyotengenezwa kwa madini ya dhahabu, shaba au fedha |
| **Miundombinu** | vitu vinavyowezesha kurahisisha upatikanaji wa huduma kama vile barabara na majengo |
| **Ufanisi** | matokeo mazuri |
| **Unasihi** | ushauri anaopewa mtu mwenye tatizo fulani |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tatu

## Kuipenda nchi yetu

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza matendo ya kuipenda nchi yetu ya Tanzania kwa kuonesha heshima kwa wimbo wa Taifa, ngao au nembo ya Taifa, bendera ya Taifa, pamoja na kutambua lugha ya Taifa na kuthamini fedha ya Taifa letu na utamaduni wa taifa. Umahiri utakaoupata katika sura hii utakuwezesha kuheshimu na kuthamini alama za taifa na kuenzi utamaduni wa taifa na hivyo kuipenda nchi yako.*

### Alama za Taifa

Vipo vitu rasmi vinavyoitambulisha Tanzania miongoni mwa mataifa mengine. Vitu hivi huitwa alama za Taifa. Je, unazifahamu alama za Taifa letu?

*Angalia picha za baadhi ya alama za Taifa letu, kisha jibu maswali.*




**Kielelezo namba 1:** *Alama za Taifa letu*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Soma majigambo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Nembo**: Mimi ni ngao ya Taifa. Ninyi wote mpo ndani yangu.

**Mwenge**: Mimi nina umbo la koni. Nawakilisha uhuru na nuru inayoangaza nchi yetu pamoja na wewe nembo.

**Bendera:** Mimi nina rangi za kupendeza. Napepea katika mlingoti.

**Nembo:** Nimejaliwa mie! Najumuisha mwanamke na mwanaume kushoto na kulia kwangu. Pembeni yao kuna mazao makuu; pamba na karafuu.

**Mwenge:** Mimi namulika mipaka, kuleta tumaini, upendo na heshima kwa watanzania wote.

**Bendera:** Mimi nina rangi nne. Sehemu ya juu nina rangi ya kijani na ya chini nina rangi ya bluu. Katikati nina mstari mweusi wenye mchirizi wa njano juu na chini.

**Nembo:** Nina mkuki, jembe na shoka, pamoja na pembe mbili za ndovu. Pia nina mlima Kilimanjaro, mlima mrefu zaidi barani Afrika. Siyo hivyo tu, pia nina maandishi yenye kaulimbiu ya Taifa “Uhuru na Umoja.”

## Zoezi la 1

1. Je, ni wapi umeshawahi kuiona nembo ya Taifa letu?
2. Ni manufaa gani ya mwenge yaliyoelezwa kwenye majigambo?
3. Eleza maana ya rangi zilizomo kwenye bendera ya Taifa letu?
4. Ni maeneo gani bendera ya Taifa hupepea?
5. Taja alama zingine za Taifa letu ambazo hazijaoneshwa katika picha.

## Kazi ya kufanya

Chora bendera ya Taifa na kisha elezea umuhimu wake.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kuthamini alama za Taifa

Katika sehemu iliyopita tulibainisha alama za Taifa. Katika sehemu hii, tutajifunza namna ya kuheshimu na kuthamini alama hizo.

*Hebu jiulize maswali yafuatayo:*

Nani mwenye wajibu wa kuthamini alama za Taifa? Ni vyema utambue kuwa ni wajibu wetu sote kuthamini alama za Taifa. Inakupasa kuthamini bendera ya Taifa, wimbo wa Taifa, fedha ya Taifa na nembo ya Taifa. Pia, mwenge wa uhuru, na mnyama wa Taifa (Twiga). Je, kwa nini tunazithamini alama hizo?

Imba wimbo huu, kisha jibu maswali yanayofuata.

**Bendera yetu**

*Bendera yetu yapepea Tanzania,*
*Ina rangi bluu nyeusi kijani na njano,*
*Inapopandishwa sote tusimame wima,*
*Inaposhushwa sote tusimame wima,*
*Tuiheshimu bendera ya Tanzania,*
*Tuzithamini alama za Tanzania.*

*Tujivunie sisi kuwa watanzania,*
*Wimbo wa Taifa lazima tuuheshimu,*
*Unapoimbwa sote tusimame wima,*
*Pia tuimbe kwa kuonesha hisia,*
*Tuzithamini alama za Tanzania.*

*Tuithamini fedha yetu ya Tanzania,*
*Na tuitunze idumu miaka mia,*
*Mwenge wa uhuru tuuthamini pia,*
*Tuukimbize na ujumbe zingatia,*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Tuzithamini alama za Tanzania.*
*Tuiheshimu nembo yetu ya Taifa,*
*Tuzingatie matumizi yake pia,*
*Tusikubali twiga kuangamia,*
*Tujivunie wetu utanzania,*
*Tuzithamini alama za Tanzania.*

**Zoezi la 2**

1. Ni matendo yapi ya kuheshimu alama za Taifa yanayotajwa katika wimbo huu?
2. Je, ni alama zipi za Taifa zilizopo shuleni kwako?
3. Je, kuna umuhimu gani wa kuthamini alama za Taifa letu?
4. Utafanya nini kwa watu wengine ili wathamini alama za Taifa?

**Kazi ya kufanya**

Angalia alama za Taifa letu zilizopo shuleni kwako. Andika matendo matatu ya kuthamini alama hizo.

FOR ONLINE USE ONLY

## Kupandishwa na kushushwa kwa bendera ya Taifa

Je, umeshawahi kuona bendera ya Taifa ikipandishwa na kushushwa? Ni muda gani bendera hiyo hupandishwa na kushushwa? Je, ni matendo gani yanayofanyika wakati wa kupandisha na kushusha bendera ya Taifa?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Mpalile ni mwanafunzi wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Mapinduzi. Vilevile, yeye ni skauti shuleni hapo. Amepewa jukumu la kupandisha na kushusha bendera ya Taifa. Huipandisha saa kumi na mbili asubuhi na huishusha saa kumi na mbili jioni kila siku. Wakati wa asubuhi, huchukua bendera na kutembea haraka kuelekea mlingotini. Mara tu afikapo hupiga hatua moja mbele kwa ukakamavu. Hufungua kamba na kuweka bendera begani, kisha hupuliza filimbi. Watu wote walio jirani husimama kwa ukakamavu na utulivu.

Baada ya hapo, Mpalile hupandisha bendera. Inapotimia saa kumi na mbili jioni, Mpalile hufika shuleni na kuelekea mlingotini kisha hupuliza filimbi. Hupiga saluti na kuanza kushusha bendera. Watu wanaopita jirani na eneo la shule wanaposikia filimbi husimama wima. Huendelea na safari baada ya bendera kushushwa. Mpalile hutoa elimu kwa wenzake juu ya taratibu za kupandisha na kushusha bendera ya Taifa. Hufanya hivyo ili atakapohitimu wanafunzi wengine waweze kubeba jukumu hilo. Kwa sasa wanafunzi wanaheshimu matendo ya kupandishwa na kushushwa kwa bendera ya Taifa.

**Zoezi la 3**

1. Umejifunza nini kutokana na habari uliyoisoma?
2. Ni matendo gani hufanyika wakati wa kupandisha bendera?
3. Ni matendo yapi yanayofanyika wakati wa kushushwa bendera?
4. Taja maeneo mengine ambapo bendera ya Taifa hupandishwa na kushushwa.
5. Utawasaidiaje wenzako wasioheshimu bendera ya Taifa?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Orodhesha kwenye daftari lako matendo yanayofanyika wakati wa kupandisha na kushusha bendera ya Taifa.

## Kupepea kwa bendera nusu mlingoti

Bila shaka umeshajifunza namna, muda na matendo yanayofanyika wakati wa kupandisha na kushusha bendera ya Taifa. Je, umewahi kuona bendera ya Taifa ikipepea nusu mlingoti? Ni wakati gani bendera hupepea nusu mlingoti? Nani mwenye mamlaka ya kuamuru bendera ya Taifa letu ipepee nusu mlingoti?

*Soma mazungumzo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Mbeta:** Kaka, nilipokuwa ninapita kituo cha polisi niliona bendera ya Taifa letu ikipepea nusu mlingoti. Kwani wameshindwa kuipandisha?

**Manyama:** Siyo kwamba wameshindwa kuipandisha, bali kuna sababu maalumu. Kwani hamjafundishwa shuleni?

**Mbeta:** Tumefundishwa kuhusu bendera ya Taifa lakini hatukufundishwa kama kuna wakati hupepea nusu mlingoti.

**Manyama:** Sawa, nitakueleza sababu za bendera kupepea nusu mlingoti.

**Mbeta:** Nitafurahi sana kaka.

**Manyama:** Bendera hupepea nusu mlingoti kwa tangazo maalumu la Rais.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mbeta:** Kumbe eeh! Nilikuwa sifahamu!

**Manyama:** Bendera ya Taifa hupepea nusu mlingoti endapo nchi itapata msiba wa kiongozi wa kitaifa. Mfano, akifariki Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu. Pia, iwapo yatatokea majanga makubwa yatakayosababisha maafa kwa watu wengi. Majanga hayo ni kama vile tetemeko la ardhi na mafuriko. Maafa hayo yatasababisha bendera kupepea nusu mlingoti.

**Mbeta:** Je, ilipotokea ajali ya meli ya MV Bukoba na kifo cha baba wa Taifa bendera ilipepea nusu mlingoti?

**Manyama:** Ndiyo! Mdogo wangu.

**Mbeta:** Asante kaka kwa kunielewesha.

**Manyama:** Asante pia kwa usikivu wako.

**Zoezi la 4**

1. Je, umejifunza nini kutokana na mazungumzo haya?
2. Ni matukio gani yanayosababisha bendera ya Taifa kupepea nusu mlingoti?
3. Je, nani hutoa tamko la bendera ya Taifa kupepea nusu mlingoti?

## Nyakati za kuimba wimbo wa Taifa

Siku zilizopita ulijifunza kuhusu bendera na nembo ya Taifa. Katika sehemu hii utajifunza kuhusu wimbo wa Taifa.

Je, unayafahamu matukio ambayo wimbo wa Taifa huimbwa? Inakupasa utambue kuwa wimbo wa Taifa hauimbwi kila wakati. Huimbwa katika matukio maalumu ambayo ni ya kitaifa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Angalia picha zifuatazo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

1.




2.



**Kielelezo namba 2:** *Nyakati za kuimba wimbo wa Taifa*

**Zoezi la 5**

1. Je, ni matendo gani yanayoonekana kwenye picha hizo?
2. Unajifunza nini kutokana na matendo hayo?
3. Je, umeshawahi kufanya matendo hayo?
4. Ni matukio gani mengine ambapo wimbo wa Taifa huimbwa?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Jadiliana na wenzako kisha mbainishe matukio matano yanayohusisha kuimbwa kwa wimbo wa Taifa. Orodhesha matukio hayo nyuma ya daftari lako.

## Utamaduni wa Taifa

Utamaduni wa Taifa ndiyo msingi wa maisha na maendeleo ya nchi. Utamaduni wa Taifa huleta umoja miongoni mwa makabila yote ya Tanzania. Je, unafahamu mambo yanayojenga utamaduni wa Taifa?

*Soma mazungumzo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Rehema na Mpoto:** Shikamoo mwalimu.

**Mwalimu**: Marahaba! Hamjambo?

**Rehema na Mpoto:** Hatujambo mwalimu!

**Rehema:** Samahani mwalimu, leo umetufundisha juu ya utamaduni wa Taifa. Ila sikuelewa vizuri ulichofundisha.

**Mpoto:** Hata mimi mwalimu sikuelewa somo la leo.

**Mwalimu:** Kwani ninyi mmeelewa nini kuhusu utamaduni wa Taifa?

**Rehema:** Mimi ninafahamu kuwa unajengwa na vitu kama utawala bora na lugha.

**Mwalimu:** Eheee! na wewe Mpoto.

**Mpoto:** Ngoja nijaribu. Unaundwa na historia ya Taifa pamoja na mila na desturi.

**Mwalimu:** Vizuri sana! Nyote mmejaribu. Utamaduni wa Taifa ni jumla ya mambo yote yanayo waunganisha watu kama Taifa. Utamaduni

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

umeunganisha makabila yote Tanzania. Vilevile, hulitambulisha Taifa kwa watu wa mataifa mengine. Pia, hujengwa na mambo kama vile nidhamu ya kazi na utu.

**Rehema:** Nimekuelewa mwalimu. Je, utamaduni wa taifa una umuhimu gani katika nchi yetu?

**Mwalimu:** Ni swali zuri sana Rehema. Kama nilivyosema mwanzo, kwamba utamaduni wa Taifa ni jumla ya mambo yote yanayowaunganisha watu kama Taifa. Pia huleta umoja na mshikamano miongoni mwa watu wa makabila tofauti. Vilevile, hujenga uzalendo miongoni mwa watanzania. Vitu vyote hivi vinasaidia kuwafanya Watanzania kuthamini na kuheshimu kazi. Pamoja na hayo, huwawezesha watanzania kujitegemea kwa kufanya shughuli mbalimbali.

**Rehema:** Hakika sasa tumekuelewa mwalimu.

**Mpoto:** Asante sana mwalimu kwa kutuelewesha vizuri.

**Zoezi la 6**

1. Unajifunza nini kutokana na mazungumzo hayo?
2. Nini hujenga utamaduni wa Taifa kutokana na mazungumzo hayo?
3. Ni mambo gani zaidi yaliyomo katika mazungumzo uliyosoma hujenga utamaduni wa Taifa?
4. Nini umuhimu wa utamaduni wa Taifa katika maendeleo ya nchi?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Lugha ya Kiswahili

Vipo vitu vinavyolitambulisha Taifa letu sambamba na alama rasmi za Taifa. Lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa vitu hivyo.

Je, unatumia lugha gani kuzungumza na wenzako? Kwa nini lugha ya Kiswahili inatumika zaidi kuwasiliana?

Mwanafunzi ni vyema utambue kuwa Kiswahili ndio lugha ya Taifa letu. Lugha hiyo hutumiwa na watu wengi kuwasiliana. Hivyo, wewe pia inakupasa kuitumia lugha hii kuwasiliana na wenzako.

Soma ngonjera ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.

*Kiswahili lugha yetu,*
*Ndiyo utamaduni wetu,*
*Chajenga mshikamano wetu,*
*Kutambulisha Taifa letu.*

*Tuitangaze lugha yetu,*
*Hata nje ya nchi yetu,*
*Tuimarishe umoja wetu,*
*Kutambulisha Taifa letu.*

*Tusiache asili yetu,*
*Kukimbilia za wenzetu,*
*Tuzungumze lugha yetu,*
*Kutambulisha Taifa letu.*

*Tuoneshe upendo wetu,*
*Kwa lugha ya Taifa letu,*
*Tuoneshe utu wetu,*
*Kutambulisha Taifa letu.*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 7**

1. Je, unajifunza nini kutokana na ngonjera hii?
2. Ni faida zipi za kutumia lugha ya Kiswahili zilizotajwa kwenye ngonjera hii?
3. Ni faida zipi nyingine unazozifahamu za kutumia lugha ya Kiswahili?
4. Je, utamsaidiaje mwenzako asiyetumia lugha ya Kiswahili mara kwa mara?

**Kazi ya kufanya**

Jadiliana na mzazi au mlezi kuhusu faida za kutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano. Andika faida tano za kutumia lugha ya Kiswahili nyuma ya daftari lako.

FOR ONLINE USE ONLY

## Kuthamini fedha

Fedha ya Tanzania ni miongoni mwa vitu vinavyolitambulisha Taifa letu. Fedha ya Tanzania inaitwa shilingi. Shilingi ya Tanzania imetengenezwa kwa noti na sarafu. Yatupasa kuthamini fedha yetu.

Je, unafanya matendo yapi ya kuthamini fedha yetu?

*Hebu tafakari matendo yafuatayo:*

1. Mwanafunzi amechora katuni kwenye fedha ya noti.
2. Mtoto amemaliza kufua na kushika fedha ya noti kabla ya kukausha mikono.
3. Mtoto amekausha mikono yake iliyokuwa na maji ili apokee fedha ya noti.
4. Mtoto amekunjakunja fedha ya noti.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Soma kisa hiki, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Zena ni mwanafunzi wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Tupendane. Yeye ni mwanafunzi mwenye nidhamu na uzalendo kwa nchi yake. Siku moja, mwalimu wa somo la Uraia na Maadili alifundisha matendo ya kuthamini fedha ya Tanzania. Zena alifurahia sana somo hilo. Wakati wa kipindi, mwalimu aliuliza "Ni matendo yapi huwa mnafanya kuthamini fedha yetu?" Wanafunzi wote walikuwa watulivu isipokuwa Zena peke yake ndiye aliyenyoosha mkono. "Eehee! Zena hebu tuambie", alisema mwalimu. Zena alijibu, "Mimi nathamini fedha kwa kuitunza kwenye pochi. Pia huwa nakausha mikono yangu kabla ya kuishika. Vilevile, huwa sikunji fedha ya noti, kuchorachora au kuchezea fedha". Mwalimu alimsifu sana Zena kwa kuwa mzalendo. Aliwataka wanafunzi wengine waige tabia ya Zena. Aliongeza kuwa, kuitunza fedha kutaifanya idumu kwa muda mrefu.

**Zoezi la 8**

1. Je, unajifunza nini kutokana na kisa hiki?
2. Ni matendo gani zaidi utakayotenda ili kutunza fedha ya noti isichakae?
3. Ni faida gani zinapatikana kwa kuthamini na kutunza fedha?
4. Je, utamshauri nini rafiki yako asiye na tabia ya kuthamini na kutunza fedha?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Jadiliana na wenzako, kisha bainisha njia tano za kutunza fedha.

**Zoezi la 9**

1. Nini faida ya kuwa na alama za Taifa?
2. Je, ni ujumbe gani unaoupata kwenye wimbo wa Taifa letu?
3. Andika habari fupi kueleza faida za kutunza fedha.

FOR ONLINE USE ONLY

**Zoezi la 10**

Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake katika kisanduku

1. Alama za Taifa la Tanzania ni pamoja na:
   - (a) Bendera ya Taifa, Mwenge wa Uhuru, Twiga
   - (b) Shoka, panga na jembe
   - (c) Mwenge, Wimbo wa shule, na Twiga ☐
   - (d) Simba, nembo, bendera ya Taifa

2. Nembo ya Taifa ina vitu vifuatavyo isipokuwa:
   - (a) Pembe za ndovu
   - (b) Pamba na mahindi
   - (c) Mwanamke na mtoto ☐
   - (d) Jembe na nyundo

3. Kutoheshimu alama za Taifa ni pamoja na:
   - (a) Kuzingatia matumizi ya nembo ya Taifa

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Kutosimama wima wakati bendera ya Taifa inapandishwa na kushushwa
(c) Kuthamini fedha ya Tanzania
(d) Kuimba wimbo wa Taifa wakati wa sherehe za kitaifa

4. ________ni jumla ya mambo yote yanayowaunganisha watu kama Taifa:
(a) Utamaduni
(b) Uzalendo
(c) Michezo
(d) Makabila

5. Matendo ya kutothamini fedha ni pamoja na:
(a) Kutokunja fedha ya noti
(b) Kuchorachora na kuchezea fedha ya noti
(c) Kushika fedha ya noti kwa mikono iliyokauka
(d) Kutunza fedha ya noti kwenye pochi

## Msamiati

**Janga** tukio baya lenye kuangamiza

**Mlingoti** mti au kifaa kinachotumika kutundikia vitu, kama vile bendera

**Mzalendo** mtu mwenye mapenzi na nchi yake

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nne

## Demokrasia

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza matendo ya demokrasia katika shule na familia. Vilevile, utajifunza utawala bora na uongozi wa kamati ya mtaa au serikali ya kijiji. Umahiri utakaoupata katika sura hii utakuwezesha kushiriki matendo ya demokrasia na kutambua muundo wa serikali za vijiji au kamati za mitaa.*

### Maana ya Demokrasia

Demokrasia ni nini? Je, Demokrasia inaundwa na mambo gani?

*Hebu fuatilia mazungumzo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Tumsifu:** Shikamoo kaka!

**Kiyando:** Marahaba! Hujambo mdogo wangu?

**Tumsifu:** Sijambo kaka! Kuna jambo linanitatiza ninaomba unisaidie.

**Kiyando:** Jambo gani hilo? Nieleze tu mdogo wangu.

**Tumsifu:** Ninaomba unieleweshe maana ya Demokrasia.

**Kiyando:** Kwani hamjafundishwa shuleni?

**Tumsifu:** Tumefundishwa lakini mwalimu ametupa kazi ya kufanya.

**Kiyando:** Ninaomba unieleze shuleni kwenu mnapataje viranja?

**Tumsifu:** Tunawachagua.

**Kiyando:** Mnawachaguaje?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Tumsifu:** Tunapiga kura.

**Kiyando:** Vizuri sana! Halafu mkishapiga kura?

**Tumsifu:** Aliyepata kura nyingi ndiye mshindi.

**Kiyando:** Basi hilo ni moja ya matendo ya kidemokrasia. Maamuzi hufanywa kwa kushirikisha watu.

**Tumsifu:** Aha! Nashukuru sasa nimeelewa.

**Zoezi la 1**

1. Umejifunza nini kutokana na mazungumzo hayo?
2. Je, Demokrasia inajengwa na nini?
3. Ni mambo gani mengine unayoyafahamu yanayojenga Demokrasia?

**Kazi ya kufanya**

Jadiliana na mwalimu juu ya aina na misingi ya Demokrasia. Andika mambo hayo nyuma ya daftari lako.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Matendo ya Demokrasia shuleni na katika jamii

Katika sehemu hii tutajifunza matendo ya Demokrasia shuleni na kwenye jamii.

*Angalia picha zifuatazo:*

1.




2.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. 

**Kielelezo namba 1:** *Matendo ya kidemokrasia*

Je, umegundua nini kutokana na picha hizo?

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Kijiji cha Msimbe ni miongoni mwa vijiji maarufu katika Wilaya ya Kingwendu. Kwanza kabisa, uongozi wa kijiji hiki ulichaguliwa na wanakijiji kwa njia ya kupiga kura. Uongozi huu umekuwa ukizingatia misingi ya sheria na haki. Wanakijiji hushirikishwa katika shughuli za maendeleo kama vile elimu, maji, na afya. Mara kwa mara, wanakijiji hupewa taarifa na hushiriki kujadili namna ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Miradi inayotekelezwa ni ujenzi wa madarasa, barabara, vituo vya afya, na uchimbaji wa visima vya maji. Wanakijiji hupewa uhuru wa kuchangia maoni yao. Pia, hukosoa kwa uwazi pale wanapoona dosari katika utekelezaji wa miradi hiyo. Vilevile, mipango ya mapato na matumizi ya kijiji imekuwa wazi kwa wanakijiji. Kuhusu elimu, serikali ya kijiji huhakikisha kuwa kila mtoto anayestahili kuanza shule anapata haki hiyo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Watoto wamekuwa wakipewa fursa sawa ya kujifunza shuleni na kushirikishwa katika maamuzi. Kwa mfano, wamekuwa wakishiriki katika kuchagua na kuchaguliwa kuwa viranja wa shule. Pia, wamekuwa wakishirikishwa katika shughuli za elimu ya kujitegemea shuleni.

**Zoezi la 2**

1. Je, ni matendo yapi ya Demokrasia yaliyotajwa kwenye habari hiyo?
2. Ni matendo yapi ya Demokrasia kati ya haya yaliyopo katika habari yanafanyika katika shule yako?
3. Ni jambo gani zuri ulilojifunza katika uongozi wa kijiji cha Msimbe?

## Utawala bora katika familia

Familia huongozwa na baba na mama au mlezi. Familia bora huwawezesha wanafamilia kushiriki katika maamuzi, kusikilizana, kusaidiana na kujadiliana. Haya ni mambo yanayojenga utawala bora katika ngazi ya familia.
Ni muhimu utawala bora uanzie katika familia zetu kwa ustawi wa Taifa letu. Familia bora hujenga Taifa imara.

*Hebu tafakari matendo yafuatayo:*

1. Mwanafunzi anamrekebisha mdogo wake anapofanya makosa.
2. Mtoto anawashirikisha wazazi wake anapofanya maamuzi.
3. Baba anamnyima mtoto chakula kwa sababu hakumwagilia bustani.
4. Wazazi hawapati muda wa kuongea na watoto wao.

Je, umegundua nini katika matendo haya?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Soma kisa hiki, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Mzee Masatu na mkewe wana watoto wanne ambao ni Kimati, Maria, Kirumo na Kilindo. Wazazi hao huhakikisha kuwa wanawapa watoto wao malezi mazuri. Huwapa mahitaji yao ya chakula, malazi na elimu. Wazazi hawa hutenga muda wa kukaa na watoto wao. Huwa wanaongea nao na kuwaelekeza mambo mbalimbali. Mfano wa mambo hayo ni jinsi ya kuishi vizuri shuleni, nyumbani na kwenye jamii. Huwafundisha watoto wao tabia njema kama utii, uwajibikaji, upendo na mshikamano. Huwashirikisha watoto wao katika maamuzi ya familia, ikiwemo mipango ya maendeleo.

Kimati na wadogo zake huwashauri wazazi wao kuhusu mipango ya baadaye ya maendeleo. Huwashirikisha wazazi wao mambo yao yote, ikiwemo ndoto zao za maisha. Wazazi nao huwapa ushauri wa jinsi ya kufanya ili kuzifikia ndoto hizo. Watoto huwajibika kikamilifu katika majukumu yote ya kifamilia. Baadhi ya majukumu hayo ni kulea wadogo zao kwa upendo. Majukumu mengine ni kushiriki kwenye usafi wa nyumbani na kuandaa chakula. Pia kushiriki kwenye shughuli za kilimo, kutunza mifugo na kusaidiana kwenye masomo.

**Zoezi la 3**

1. Je, ni matendo gani yanayoonesha utawala bora kwenye kisa hiki?
2. Taja matendo yanayofanana na hayo ambayo ungependa yafanyike katika familia yenu?
3. Je, familia ya Masatu itapata faida zipi kwa kutenda matendo hayo?
4. Je, wewe unaweza kufanya nini kurekebisha ukosefu wa utawala bora ndani ya familia?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Jadiliana na wazazi au walezi kuhusu mambo ya kufanya ili kudumisha utawala bora katika familia. Andika mambo hayo kwenye daftari lako.

## Uongozi wa kamati ya mtaa na serikali ya kijiji

Serikali hutoa huduma za kijamii kwa wananchi wake. Ili wananchi wapate huduma bora ni muhimu huduma zianzie katika kamati ya mtaa au serikali ya kijiji.

Unawafahamu viongozi wa kamati ya mtaa au serikali ya kijiji? Unafahamu namna wanavyopatikana?

*Hebu fuatilia mazungumzo haya, kisha ujibu maswali yanayofuata.*

**Mtanga:** Shikamoo babu!

**Mzee Sijaona:** Marahaba! Hujambo mjukuu?

**Mtanga:** Sijambo. Samahani babu, nina maswali naomba nikuulize.

**Mzee Sijaona:** Uliza tu mjukuu wangu.

**Mtanga:** Babu, kuna tofauti gani kati ya mtaa na kijiji?

**Mzee Sijaona:** Mtaa upo ndani ya mji au jiji, lakini kijiji ni eneo lililopo nje ya mji.

**Mtanga:** Je, muundo wa mtaa ukoje?

**Mzee Sijaona:** Mtaa huundwa na kaya zisizopungua hamsini. Vilevile, kila mtaa huongozwa na kamati ya mtaa.

**Mtanga:** Je, muundo wa kamati ya mtaa ukoje?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mzee Sijaona:** Kamati ya mtaa inaundwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa. Huongozwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Mtaa, Ofisa Mtendaji wa Mtaa, na wajumbe wengine sita. Wajumbe hao ni wenyeviti wa kamati ndogo ndogo. Kamati hizi husimamia ulinzi na usalama, afya na ustawi wa jamii, uchumi na fedha. Pia, husimamia elimu na miundombinu kama vile maji, barabara na umeme. Vilevile, ipo kamati ndogo ya maafa.

**Mtanga:** Je, viongozi hao hupatikanaje?

**Mzee Sijaona:** Mwenyekiti wa kamati ya mtaa na wajumbe sita huchaguliwa na wakazi wa mtaa husika wenye sifa ya kupiga kura. Uchaguzi huo hufanyika kila baada ya miaka mitano. Ofisa Mtendaji wa Mtaa huajiriwa na halmashauri ya mji, manispaa au jiji. Mwenyekiti wa mtaa ndiye msimamizi mkuu wa shughuli zote kwenye mtaa. Ofisa Mtendaji ni katibu wa vikao vya kamati ya mtaa.

**Mtanga:** Babu, na muundo wa kijiji nao ukoje?

**Mzee Sijaona:** Kijiji huundwa na vitongoji kadhaa ambapo kila kitongoji huongozwa na mwenyekiti. Vilevile, kila kijiji huongozwa na serikali ya kijiji. Serikali ya kijiji nayo inaundwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa. Viongozi wa juu ni mwenyekiti wa kijiji na Ofisa Mtendaji wa kijiji. Viongozi wengine ni wajumbe wa kamati za serikali ya kijiji. Viongozi hawa pia

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

hupatikana kila baada ya miaka mitano.

**Mtanga:** Asante babu sasa nimeanza kuelewa. Je, nini umuhimu wa kamati ya mtaa au serikali ya kijiji?

**Mzee Sijaona:** Kamati ya mtaa au serikali ya kijiji inasimamia kwa karibu maendeleo ya wananchi. Inawezesha upatikanaji wa rasilimali ardhi, huduma bora za maji, elimu, afya, na barabara. Pia, inachochea ukuaji wa viwanda kupitia shughuli za kilimo, uvuvi, na ufugaji.

**Mtanga:** Ninashukuru babu kwa kunielewesha vizuri. Sina tena cha kuuliza.

**Mzee Sijaona:** Ninafurahi kuwa umenielewa vyema. Nakusihi uendelee kuwa mdadisi kwa mambo usiyoyafahamu.

## Zoezi la 4

1. Nini tofauti kati ya mtaa na kijiji?
2. Nini umuhimu wa kamati ya mtaa na serikali ya kijiji?
3. Viongozi gani wa kamati ya mtaa na serikali ya kijiji huchaguliwa na wananchi?

## Kazi ya kufanya

Tembelea ofisi za mtaa au kijiji, uliza muundo wa uongozi na majukumu yake. Andika majibu kwenye daftari lako.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5

1. Eleza matendo ya Demokrasia yanayofanyika shuleni kwenu.
2. Orodhesha matendo matatu ya utawala bora yanayofanyika kwenye familia yako.
3. Taja faida nne za Demokrasia katika familia.
4. Orodhesha matatizo manne yatakayotokea ikiwa wanafunzi hawachagui viongozi wao na hawana uhuru wa kujieleza.

## Zoezi la 6

Oanisha maneno katika **sehemu A** kwa kuchagua majibu katika **sehemu B**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| i. Demokrasia | (a) Eneo lililoko nje ya mji |
| ii. Utawala bora katika familia | (b) Kuwajengea wananchi nyumba za kuishi |
| iii. Kazi mojawapo ya serikali ya kijiji | (c) Wazazi kuwashirikisha watoto wao kufanya maamuzi katika masuala ya kifamilia |
| iv. Kamati ya mtaa | (d) Kiongozi kuteuliwa na mtu mmoja |
| | (e) Kiongozi kuchaguliwa kwa kupiga kura |
| | (f) Watoto hawaruhusiwi kushiriki katika kufanya maamuzi ya masuala ya kifamilia |
| | (g) Kuhakikisha wanakijiji wanapata huduma za kijamii kama vile maji, umeme, barabara |
| | (h) Eneo lililopo mjini |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Msamiati

| | |
|---|---|
| **Demokrasia** | mfumo wa utawala ambapo wananchi hushirikishwa katika maamuzi |
| **Kamati** | kikundi cha watu kinachoundwa kufanya kazi fulani |
| **Kitongoji** | eneo dogo lililopo katika kijiji. |
| **Kushirikishwa** | kupewa nafasi ya kutoa mchango wa mawazo na kutenda. |
| **Mtaa** | eneo dogo la utawala lililopo mjini. |
| **Utawala bora** | kuongoza kwa kuzingatia ushirikishaji wa watu katika maamuzi. |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tano

## Kujijali na kuwajali watu wengine

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza matendo ya kujali na kujenga uhusiano mwema na wenzako. Pia, utajifunza matendo yanayoepusha tabia hatarishi kwa afya yako, familia na jamii. Vilevile, utajifunza utunzaji wa mazingira katika jamii kama njia ya kujilinda na kuilinda jamii. Umahiri utakaoupata katika sura hii utakuwezesha kujiepusha na tabia hatarishi zinazoathiri afya. Vilevile, utakuwezesha kutoa elimu kuhusu utunzaji wa mazingira katika jamii.*

### Matendo ya mtu anayejijali

Katika maisha ya kila siku, kuna matendo mbalimbali unayoweza kufanya ili kuonesha kuwa unajijali.

Ni kwa namna ipi unamtambua mtu anayejijali? Ni kwa namna gani unajiepusha na tabia zinazoweza kuhatarisha maisha yako?

*Hebu tafakari matendo yafuatayo:*

1. Mwanafunzi anafanya mazoezi ya viungo kila siku asubuhi na jioni.
2. Mtoto anashusha chandarua kabla ya kulala.
3. Mwanafunzi wa kike anamsimulia baba yake jinsi anavyoepuka kushawishiwa kufanya ngono na kijana wa kiume.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Je, umegundua nini kutokana na matendo haya? Katika maisha ya kila siku yapo matendo mbalimbali ya kujijali unayoweza kufanya. Je,wewe unajijali kwa namna gani?

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Dora ni mwanafunzi wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Chekereni. Kila asubuhi huamka mapema na kufanya mazoezi ya viungo. Hii humfanya awe na nguvu na mkakamavu. Husafisha chumba chake, hukipanga vizuri na hutandika kitanda chake. Baadaye hupiga mswaki na kuoga. Wazazi wake humpatia chakula chenye virutubisho vya kutosha ili awe na afya njema.

Siku moja walipokuwa wanacheza kwenye uwanja wa shule alikuja kijana mmoja. Kijana huyo alitaka kuwapatia biskuti na peremende. Rafiki yake Dora alitaka kupokea zile peremende na biskuti. Dora alimsihi asipokee vitu kutoka kwa mtu asiyemjua. Kijana huyo alizidi kuwashawishi. Dora alitoa taarifa kwa mwalimu juu ya kuwepo kwa kijana mgeni maeneo ya shule. Mwalimu alitoka ofisini na kwenda pale alipokuwa, kijana. Naye kijana alipoona mwalimu anakuja alianza kukimbia. Kabla hajafika mbali wanafunzi wakamkamata. Yule kijana alipelekwa kwenye ofisi ya mwalimu mkuu na kuhojiwa. Mwalimu mkuu alimwambia, “Loh! Kumbe wewe ni kijana hatari sana. Unawarubuni wasichana kwa zawadi ili kuwaingiza katika tabia za kupenda ngono”.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 1**

1. Je, ni matendo gani ya kujijali uliyojifunza kutoka kwa Dora?
2. Unafanya matendo gani ya kujijali zaidi ya haya yaliyotajwa kwenye habari?
3. Je, utamshauri nini rafiki yako asiyejijali?
4. Taja faida unazozipata kwa kufanya matendo ya kujijali.
5. Je, ungekuwa Mwalimu mkuu ungewaeleza nini wanafunzi ili waweze kujijali?

**Kazi ya kufanya**

Andika orodha mbili za matendo ya kujijali utakayotenda kwa wiki nzima. Orodha ya kwanza ioneshe matendo ya kujijali utakayofanya shuleni. Orodha nyingine ioneshe matendo ya kujijali utakayofanya ukiwa nyumbani.

## Tabia na mienendo hatarishi

Kujihakikishia usalama wako ni ishara ya kujijali. Hivyo ili uwe salama, unapaswa kujiepusha na vitendo hatarishi.

Ni kwa namna gani utaweza kuepuka vitendo hatarishi? Je, utawaepushaje wanafamilia na wanajamii wenzako dhidi ya vitendo hatarishi?

*Hebu tafakari tabia zifuatazo:*

1. Mwanafunzi anacheza kwenye mtaro wa maji machafu.
2. Mwanafunzi anakaa kijiweni na watu wanaovuta bangi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1. Mwanafunzi ana marafiki ambao ni wezi.
2. Msichana amevaa nguo fupi iliyoacha wazi sehemu kubwa ya mwili wake.
3. Mtoto anapenda kuzurura nyakati za usiku.
4. Mtoto hazingatii kanuni za usafi anapotoka chooni.

*Soma mahojiano baina ya Juma na Maria, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Juma:** Habari za siku Maria!

**Maria:** Nzuri tu Juma! Hivi ukitoka shuleni huwa unafanya nini?

**Juma:** Nikitoka shuleni, huenda kwa rafiki zangu kuongea na kujifurahisha.

**Maria:** Huwa unatumia muda gani kufika nyumbani?

**Juma:** Nikitoka shuleni saa nane mchana, hufika nyumbani saa mbili usiku.

**Maria:** Ina maana unazurura hadi muda huo?

**Juma:** Ndiyo!

**Maria:** Unafurahia kufanya hivyo?

**Juma:** Ndiyo! Ninafurahi, kwani wewe hutembelei wenzako?

**Maria:** Hapana Juma! Nikitoka shuleni huenda nyumbani moja kwa moja.

**Juma:** Kwa nini hupendi kuwa na wenzako baada ya shule?

**Maria:** Ni hatari kuzurura baada ya muda wa masomo.

**Juma:** Kwani kuna hatari gani?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Maria:** Kuna hatari ya kukutana na magenge ya wahalifu au walevi muda huo.

**Juma:** Kweli Maria! Hata mimi ninawaogopa watu hao.

**Maria:** Basi unapaswa kuachana na tabia hiyo. Ukitoka shuleni nenda nyumbani na uwasaidie wazazi kufanya kazi mbalimbali za nyumbani.

**Juma:** Asante Maria! Nitawashauri wenzangu nao wafanye hivyo.

## Zoezi la 2

1. Je, ni tabia zipi hatarishi ulizozisoma katika mahojiano?
2. Ni tabia gani nyingine hatarishi unazozifahamu zaidi ya ulizozisoma katika mahojiano?
3. Maria ameonesha tabia gani katika mahojiano?
4. Ni tabia gani kati ya tabia za Maria au Juma zinazofaa kuigwa?
5. Ukiwa na marafiki wenye tabia kama ya Juma, utawashauri nini?

## Kazi ya kufanya

Chunguza matendo hatarishi yanayofanywa na watoto katika eneo unaloishi. Orodhesha matendo yaliyojitokeza mara nyingi zaidi. Andika namna utakavyowasaidia ili wasiendelee kutenda matendo hayo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Madhara ya ngono za utotoni na dawa za kulevya

Umejifunza kuhusu tabia hatarishi katika sehemu iliyopita. Zipo tabia nyingi hatarishi. Miongoni mwa tabia hizo ni kushiriki katika ngono za utotoni, na utumiaji wa dawa za kulevya.

Ni kwa namna gani watoto hujiingiza katika tabia za ngono na utumiaji wa dawa za kulevya? Umeshawahi kusikia au kuwaona watoto wenye tabia hizo? Je, walipata madhara gani?

*Soma mahojiano yafuatayo kati ya mama na watoto, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Watoto:** Shikamoo mama!

**Mama:** Marahaba wanangu! Habari za shule?

**Watoto:** Nzuri mama!

**Mama:** Leo mmejifunza nini?

**Mikidadi:** Tumejifunza juu ya tabia hatarishi kwa watoto, familia na jamii.

**Lusi:** Hivi mama, watoto wanaweza kujiingiza kwenye tabia za ngono?

**Mama:** Ndiyo Lusi! Inawezekana kabisa.

**Mikidadi:** Ahh, mama! Inawezekanaje?

**Mama:** Mnakumbuka kuwa nimewaambia msipokee fedha au zawadi toka kwa watu msiowajua?

**Watoto:** Ndiyo mama! Tunakumbuka.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mama:** Wapo watu wanaowalaghai watoto kwa kuwapa fedha au zawadi. Baadaye huwashawishi kuingia kwenye vitendo vya ngono.

**Mikidadi:** Kumbe!

**Lusi:** Mama kuna madhara gani ya kujihusisha na vitendo vya ngono za utotoni?

**Mama:** Yapo madhara mengi kama vile kupata mimba za utotoni. Pia, kuambukizwa magonjwa ya zinaa.

**Lusi:** Nimeelewa mama. Mwalimu pia alizungumzia kuhusu matumizi ya dawa za kulevya.

**Mama:** Hiyo pia ni tabia hatarishi sana kwani dawa za kulevya ni hatari kwa afya.

**Mikidadi:** Je, kuna tabia gani nyingine zenye madhara?

**Mama:** Wapo watoto wanaoingia kwenye makundi ya ulevi wa pombe na uvutaji sigara.

**Mikidadi:** Kweli mama! Mwalimu alitusihi tusizurure mitaani na tujiepushe na makundi ya watoto wenye tabia hizo.

**Mama:** Watoto wanaokaa vijiweni wapo katika hatari ya kujihusisha na dawa za kulevya. Kama unajipenda lazima ujiepushe na makundi hayo.

**Watoto:** Asante mama! Tutayazingatia yote.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 3**

1. Je, ni tabia gani hatarishi zilizotajwa kwenye mazungumzo haya?
2. Je, wanafunzi wanaojihusisha na tabia hizo hupata madhara yapi?
3. Ni kwa namna gani unaweza kujiepusha na tabia hatarishi?
4. Utamshauri nini rafiki yako anayejihusisha na tabia hatarishi?

**Kazi ya kufanya**

Jadiliana na mwalimu wa unasihi kuhusu madhara ya ngono za utotoni na dawa za kulevya. Andika habari fupi kuhusu majadiliano hayo kwenye daftari.

## Kutunza rasilimali za familia

Katika darasa la tatu ulijifunza kuwa rasilimali ni vitu vinavyoweza kutumiwa ili kutuletea maendeleo. Hebu tazama mazingira ya nyumbani kwenu. Unaona rasilimali gani?

Je, wewe unatunzaje rasilimali za familia? Rasilimali za familia zinapotunzwa hudumu. Kila familia ina rasilimali zake. Inakupasa kujifunza namna ya kuzitunza na kuzitumia vizuri. Ni kwa namna gani unazitunza?

*Hebu tafakari matendo yafuatayo:*

1. Mtoto anamwaga chakula kilichobaki jana.
2. Mtoto amepakua chakula kingi kuliko wenzake na ameshindwa kukimaliza.
3. Taa zinawaka vyumbani kukiwa hakuna mtu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1. Mtoto ametumwa dukani na ametumia fedha iliyobaki kununua peremende bila ridhaa ya wazazi au mlezi.
2. Mtoto amefungua bomba na kuacha maji yakimwagika.

Je, matendo hayo yanaonesha nini? Wewe unatenda matendo hayo katika familia yako?

*Soma majadiliano yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Mwalimu Debora huwafundisha wanafunzi wake umuhimu wa kutunza rasilimali. Siku moja aliendesha mjadala juu ya utunzaji wa rasilimali za familia.

**Mwalimu:** Ni kwa namna gani tunatunza rasilimali za familia?

**Yusufu:** Unapotoka chumbani ni vyema kuzima taa ili kupunguza gharama za umeme.

**Mwalimu:** Umejibu vyema Yusufu. Hii ni njia mojawapo ya kutunza rasilimali. Je, ipi ni njia nyingine?

**Yakobo:** Njia nyingine ni matumizi bora ya maji. Kila tunapofungulia maji ni vyema kuyafunga ili yasitiririke ovyo.

**Mwalimu:** Ni kweli Yakobo! Hii itawasaidia wazazi kupunguza malipo makubwa ya ankara za maji. Selina, ni lipi jambo jingine?

**Selina:** Mara nyingi watu hupakua chakula kingi na kushindwa kukimaliza. Huu pia ni uharibifu wa rasilimali.

**Mwalimu:** Umejibu vizuri sana. Ni vizuri kupakua chakula unachoweza kukimaliza. Yusufu una cha kuongeza?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Yusufu:** Jambo jingine ni matumizi mazuri ya fedha. Wakati mwingine tunanunua vitu tusivyovihitaji. Haya ni matumizi mabaya ya rasilimali kwenye familia.

**Yakobo:** Aha kumbe! Nitawashauri wazazi kuweka mpango maalumu wa matumizi ya fedha.

**Selina:** Mimi nimefaidika na huu mjadala wa leo. Nimebaini umuhimu wa kutunza rasilimali za familia.

### Zoezi la 4

1. Umejifunza nini kutokana na mjadala huu?
2. Ni tabia zipi zinachangia matumizi mabaya ya rasilimali za familia?
3. Taja tabia zaidi ya zilizotajwa kwenye majadiliano ambazo huchangia matumizi yasiyofaa ya rasilimali.

### Kazi ya kufanya

Jadiliana na wenzako kuhusu matumizi ya rasilimali za nyumbani. Chora jedwali linaloonesha matendo ya matumizi mazuri na mabaya ya rasilimali. Kisha onesha kwa idadi matendo hayo kama yalivyojitokeza. Zingatia mfano ufuatao:

*Mfano wa jedwali*

| Siku za wiki | Matendo | Idadi ya kutokea |
|---|---|---|
| Jumatatu | Kuacha pasi inawaka | 3 |

Baada ya juma moja, waeleze wazazi au walezi juu ya matokeo uliyoyapata.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Utunzaji wa mazingira

Mazingira hujumuisha maeneo tunayoishi na vitu vinavyo tuzunguka. Uharibifu wa mazingira husababishwa na tabia na mienendo isiyofaa. Katika sehemu hii utajifunza kubaini tabia na mienendo inayoleta uharibifu wa mazingira. Pia, utajifunza namna ya kutoa elimu juu ya utunzaji wa mazingira. Vilevile, utajifunza namna ya kushiriki kutunza mazingira katika jamii.

## Tabia na mienendo inayoleta uharibifu wa mazingira katika jamii

Je, unafahamu tabia na mienendo inayoleta uharibifu wa mazingira katika eneo unaloishi?

*Hebu tafakari matendo yafuatayo:*

1. Abiria anatupa takataka barabarani.
2. Wananchi wanatupa mifuko ya takataka kwenye mifereji na mitaro ya maji.
3. Wanafunzi wanajisaidia haja ndogo kwenye kuta za majengo ya shule.
4. Wananchi wameweka mabomba yanayotiririsha maji machafu kutoka majumbani mwao kwenda kwenye mto.
5. Gari la takataka linatembea huku likimwaga takataka barabarani.

Je, umegundua nini katika matendo hayo?

*Soma kisa kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Kijiji cha Itaga kipo mkoani Tabora. Miaka ya nyuma kijiji hiki kilikuwa na miti mingi. Ilikuwepo mito ya maji iliyotiririka kutokea milimani kwenda mabondeni. Pia, kulikuwepo na vyanzo vya

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

maji vilivyofunikwa na misitu minene. Wakazi wake walipenda kukaa chini ya vivuli vya miti wakijipumzisha. Mvua za kutosha zilikuwa zinanyesha kila msimu. Walilima mashamba yao na kuvuna mazao ya kutosha. Walifuga na kulisha mifugo bila shida. Hata hivyo, baada ya miaka mingi kupita watu waliongezeka sana. Je, unajua nini kilitokea? Watu walikata miti ili kujenga nyumba zao. Walitengeneza samani na kujenga nyumba kwa kutumia mbao. Pia, wakachoma misitu ili kupata mkaa. Loh! Kijiji kilibadilika sana na maisha yalibadilika pia. Wakazi wa kijiji cha Itaga walikata miti sehemu za vyanzo vya maji. Hivyo, misitu ilipungua sana. Watu wanajisaidia kwenye mito na kutupa takataka kila mahali. Hali hii ilisababisha kuwepo kwa magonjwa kijijini hapo.

## Zoezi la 5

1. Ni mambo gani ya uharibifu wa mazingira yaliyopo kwenye kisa hiki?
2. Ni vitendo gani vya uharibifu wa mazingira vinafanyika kwenye mazingira yako?
3. Ni magonjwa gani yanayoweza kutokea kwenye kijiji cha Itaga?
4. Ni nini athari za uharibifu wa mazingira kwenye kilimo na ufugaji?
5. Ni vitendo vipi vya utunzaji wa mazingira unavyovifahamu?

## Kazi ya kufanya

Zungumza na mwalimu wa mazingira ili kubainisha vitendo vya uchafuzi wa mazingira shuleni. Aidha, mjadili njia za kutunza mazingira hayo. Andika vitendo hivyo na njia zilizobainishwa kwenye daftari lako.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Shughuli za usafi wa mazingira yetu

Bila shaka sasa umejifunza stadi za utunzaji wa mazingira. Je, ni kwa namna gani unashiriki katika usafi wa mazingira kwenye eneo unaloishi?

*Angalia picha zifuatazo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

1. 

2. 

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3.



4.




**Kielelezo namba 1:** *Shughuli za kutunza mazingira*

## Zoezi la 6

1. Je, picha hizi zinaonesha matendo gani kuhusu mazingira?
2. Je, unashiriki katika matendo gani ya usafi wa mazingira nyumbani na shuleni?
3. Utafanya nini kuwahamasisha wenzako kutunza mazingira?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Jadiliana na wenzako namna ya kushiriki katika shughuli za usafi wa mazingira katika eneo mnaloishi. Orodhesha shughuli mtakazofanya. Kisha, andaa ratiba ya ushiriki wenu siku za mwisho wa wiki.

## Elimu ya utunzaji wa mazingira

Umeshajifunza kuhusu mazingira, uharibifu unaofanyika, pamoja na madhara ya uharibifu wa mazingira. Hebu jiulize umechukua hatua gani za kuzuia uharibifu huo? Unawasaidiaje rafiki zako wasiharibu mazingira katika eneo unaloishi?

*Soma kisa kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Juma na Samia ni wanafunzi katika Shule ya Msingi Michungwani. Shule hiyo ipo katika Kijiji cha Michungwani, wilaya ya Handeni. Kijiji hicho kimeathirika na uharibifu wa mazingira. Mwalimu wa Uraia na Maadili aliwafundisha stadi mbalimbali za utunzaji wa mazingira. Juma na Samia walijiunga na klabu ya mazingira iliyopo shuleni kwao. Huko walijifunza pia namna ya kutumia vifaa vya kusafishia mazingira. Waliamua kutumia stadi hizo kuwaelimisha wanakijiji namna ya kutunza mazingira yao. Siku moja Juma na Samia walimtembelea mwenyekiti wa kijiji. Walimweleza nia yao ya kuwaelimisha wanakijiji kuhusu utunzaji wa mazingira. Mwenyekiti aliitikia wito wao. Siku iliyofuata mwenyekiti aliitisha mkutano wa wanakijiji wote. Samia na Juma walifika kwenye mkutano pamoja na kiongozi wa klabu ya mazingira. Pia mwalimu wa mazingira kutoka shuleni kwao alihudhuria. Walitoa elimu ya mazingira kwa wanakijiji. Waliwaelimisha wanakijiji kuhusu



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

umuhimu wa kufyeka nyasi, kuchoma takataka, na kutunza vyanzo vya maji. Aidha, waliwaelimisha kuhusu kusafisha mitaro ya maji na kuondoa taka katika makazi yao. Wanakijiji walikubaliana kusafisha mazingira ya kijiji chao kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi.

### Zoezi la 7

1. Ni njia gani ulizojifunza za kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira?
2. Upi ni mchango wa Juma na Samia kuhusu utunzanji wa mazingira katika kijiji chao?
3. Ni tabia ipi ya kuigwa kwenye kisa hiki?
4. Je, wewe utafanya nini katika utoaji wa elimu ya mazingira kwenye eneo unaloishi?
5. Je, kijiji cha Michungwani kitapata faida gani kutokana na elimu ya utunzaji wa mazingira?

### Kazi ya kufanya

Jadiliana na wanafunzi wenzako, mpange namna ya kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira. Elimu hiyo itolewe katika jamii mwishoni mwa wiki. Mshirikiane na mwalimu wa somo la Uraia na Maadili na mwalimu wa mazingira.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 8

1. Je, ni vitendo vipi hatarishi vinavyofanywa na wanafunzi wa shule yako?
2. Andika njia tano za kuepuka vitendo hatarishi kwa mtoto.
3. Orodhesha madhara ya ngono za utotoni.
4. Taja rasilimali tatu za familia unazozifahamu.
5. Je, utafanya nini kuzuia uharibifu wa mazingira shuleni kwenu?

## Zoezi la 9

Andika **ndiyo** kwenye sentensi sahihi au **hapana** kwenye sentesi isiyo sahihi.

1. Kunawa mikono kwa maji na sabuni kabla ya kula ni tendo la kujijali__________.
2. Kushiriki ngoma za usiku ni tabia hatarishi_________.
3. Kutupa takataka kwenye mto ni kitendo cha utunzaji mazingira__________.
4. Kuharibu misitu kwa kuchoma moto na kukata miti husababisha ukame___________.

## Msamiati

| | |
|---|---|
| **Kilevi** | kitu kinacholewesha |
| **Kudadisi** | kuchunguza jambo au kuhoji |
| **Kurubuni** | kushawishi kwa kulaghai |
| **Mienendo** | mazoea ya utendaji wa jambo |
| **Rasilimali** | vitu vya thamani alivyonavyo mtu au nchi |
| **Tabia hatarishi** | tabia inayoweza kukuletea madhara |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Sita

## Kuwajibika na kulinda rasilimali

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza tabia ya kujitolea katika jamii yako. Pia, utajifunza kujenga tabia ya kuthamini rasilimali za jamii na kutimiza wajibu wako katika familia. Mwisho utajifunza kushirikiana na wengine kutekeleza majukumu ya nyumbani na shuleni. Umahiri utakaoupata katika sura hii utakuwezesha kuzitambua na kuzilinda rasilimali kwa maslahi ya nchi.*

### Kutimiza wajibu katika familia

Je, huwa unatekeleza majukumu gani ukiwa nyumbani? Ni vyema ukatambua kuwa kutekeleza majukumu ndio kutimiza wajibu. Hali hii huitwa uwajibikaji.

Inakupasa utambue kuwa ni wajibu wako kufanya shughuli mbalimbali katika familia. Moja ya shughuli unazopaswa kufanya katika ngazi ya familia ni kulea wadogo zako. Pia, kutunza mali za familia na kushiriki katika shughuli za maendeleo za familia. Vilevile, ni vyema kuwahudumia wazazi na ndugu wanapopatwa na matatizo mfano, ugonjwa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Angalia picha hizi, kisha jibu maswali yanayofuata.*

1.



2.



3.



FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4.



**Kielelezo namba 1:** *Matendo ya kuwajibika katika familia*

**Zoezi la 1**

1. Umebaini matendo yapi katika picha hizi?
2. Ni matendo gani unayotenda kutekeleza wajibu wako katika familia?
3. Unajisikiaje unaposhindwa kutekeleza wajibu wako katika familia?
4. Utafanya nini ikiwa utashindwa kutimiza wajibu wako katika familia?

**Kazi ya kufanya**

Waulize wazazi au walezi, wakueleze wajibu wako katika familia. Andika katika daftari lako namna utakavyotekeleza wajibu wako.

## Kushiriki shughuli ndogondogo kwenye familia

Katika familia zipo shughuli unazoweza kuzifanya. Shughuli hizi ni kama vile, kufagia uwanja wa nyumba, na kunyoosha nguo. Nyingine ni kudeki nyumba na kuchoma takataka. Ni shughuli gani unazozifanya katika familia yako? Unajisikiaje unapofanya shughuli hizo?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Angalia picha zifuatazo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

1. 

2. 

3. 

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4.



5.



**Kielelezo namba 2:** *Watoto wanafanya shughuli ndogondogo kwenye familia*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 2**

1. Je, ni shughuli gani zinazoonekana katika picha?
2. Kati ya shughuli hizo, ni zipi unazozifanya katika familia?
3. Taja shughuli nyingine zaidi ya hizo zinazoonekana kwenye picha unazoweza kufanya katika familia yenu.

**Kazi ya kufanya**

Orodhesha shughuli zinazofanyika katika familia yako. Andika orodha ya shughuli zako kwa juma zima. Kisha, kabidhi orodha hiyo kwa mwalimu wa somo.

## Kujitolea katika jamii

Miongoni mwa matendo ya kuwajibika ni kujitolea kufanya kazi mbalimbali. Kazi hizi zina manufaa kwako na jamii kwa ujumla. Je, umewahi kufanya shughuli za kujitolea shuleni au nyumbani? Ni shughuli zipi za kujitolea unazoweza kufanya katika jamii yako?

*Soma kisa hiki, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Tito ni mtoto hodari na mzalendo. Tito anasoma darasa la nne katika shule ya msingi Kaliwa. Tito anapendwa na walimu, wazazi na jamii inayomzunguka. Pia ni mlezi mzuri wa wadogo zake. Vilevile, hushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii siku za mwisho wa juma. Shughuli hizo ni kukata nyasi, kuondoa takataka kwenye maeneo ya wazi na kuzichoma. Pia hupalilia bustani za maua shuleni na nyumbani bila kuambiwa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tito amejiunga na kikundi cha utunzaji wa mazingira kwenye eneo analoishi. Kikundi hicho hutoa elimu ya mazingira, huotesha miti na kuitunza. Eneo analoishi Tito linavutia sana. Aidha, amejiunga na klabu ya elimu ya amani shuleni. Klabu hii hutoa elimu ya amani ndani na nje ya shule. Elimu hiyo inahusu namna ya kuishi na watu tofauti. Pia namna ya kuwajali watu na kuvumilia watu wengine. Kazi hii hufanywa bila malipo. Kikundi hiki kimesaidia kupunguza migogoro shuleni na kwenye jamii.

## Zoezi la 3

1. Je, ni tabia gani inayooneshwa na Tito katika kisa hiki?
2. Je, una maoni gani kuhusu tabia inayooneshwa na Tito?
3. Taja shughuli za kijamii ambazo ungependa kujitolea kushiriki.
4. Shughuli za kujitolea zina manufaa gani katika jamii?

## Kazi ya kufanya

Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu shughuli za kujitolea katika jamii. Chora jedwali la shughuli za kujitolea ambazo ungependa kuzifanya mwishoni mwa juma. Kisha onesha kwa idadi matendo utakayofanya.

*Mfano wa jedwali*

| Siku za wiki | Matendo | Idadi ya kujitolea |
|---|---|---|
| Jumamosi | Kushiriki usafi wa mazingira | 2 |

Wasilisha jedwali hilo kwa mwalimu wa Uraia na Maadili.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kuthamini rasilimali za jamii

Baada ya kujifunza tabia ya kujitolea katika jamii, sasa utajifunza tabia ya kuthamini rasilimali za jamii.

*Utachukua hatua gani ikiwa:*

1. Wanafunzi wenzako wanapasua bomba ili wachote maji.
2. Mwanafunzi mwenzako anachora katuni ukutani.
3. Mwanafunzi anajisaidia nje ya maliwato?

*Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Kijiji cha Jumbo kinaheshimika kwa utunzaji wa rasilimali zake. Rasilimali hizo ni majengo, barabara, mabomba ya maji, misitu, ardhi, na vyanzo vya maji. Wanakijiji hawa wamejiwekea utaratibu mzuri wa utunzaji wa rasilimali zao. Kwa mfano, hairuhusiwi kuchafua vyanzo vya maji na kukata miti ovyo. Vilevile, hairuhusiwi kuchoma misitu, kuharibu majengo na barabara za kijiji.

Kijiji hicho kinapata mvua za muda mrefu. Kuna misitu mikubwa na inayovutia. Mito yao hutiririsha maji muda wote kwa mwaka mzima. Barabara zao hupitika muda wote na wanakijiji wamenufaika na biashara ya mazao. Mwenyekiti wa kijiji hutoa elimu ya kutunza na kuendeleza rasilimali za kijiji chake. Katika kikao cha wenyeviti wa vijiji, mwenyekiti wa kijiji cha Jumbo alipewa zawadi.

Tofauti na kijiji cha Jumbo, wakazi wa kijiji cha Makendo hawatunzi rasilimali za kijiji chao. Barabara zina mashimo makubwa na misitu imepungua sana. Ardhi ya kijiji hiki haina rutuba na vyanzo vyote vya maji vimekauka. Biashara ni ngumu kufanyika kutokana na ubovu wa barabara.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 4**

1. Je, mafanikio waliyonayo wanakijiji wa Jumbo yametokana na nini?
2. Kwa nini mwenyekiti wa Jumbo alipewa zawadi?
3. Je, ni rasilimali gani nyingine zinazothaminiwa katika jamii yako?
4. Ni madhara gani ya uharibifu wa mazingira yamejitokeza katika kijiji cha Makendo?
5. Je, unapenda kumshauri nini mwenyekiti wa kijiji cha Makendo?

**Kazi ya kufanya**

Chunguza mtaa au kijiji chako, kisha uorodheshe rasilimali zilizopo na jinsi zinavyotunzwa.

FOR ONLINE USE ONLY

## Kushirikiana kutekeleza majukumu ya shuleni na nyumbani

Kuna faida nyingi zinazopatikana kwa kushirikiana na wenzako. Unatakiwa ujenge tabia ya kushirikiana na watu tofauti. Utaweza kujifunza mambo mengi kwa kushirikiana na watu wengine.

Je, unashirikiana na watu gani kwenye kazi zako za kila siku? Je, unashirikiana vipi na wenzako?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Soma shairi hili, kisha jibu maswali yanayofuata.

*Roda, Doto nae Pili, marafiki wa ukweli,*
*Bidii kwao kamili, masomo wafanya kweli,*
*Masomo wanahimili, na makundi mbalimbali,*
*Ushirika muhimili, kwenye mambo mbalimbali.*

*Uraia Maadili, Roda ni kipaji chake,*
*Kucheza ngoma mahiri, hakuna mfano wake,*
*Sayansi teknolojia, Pili ni nafasi yake,*
*Ushirika muhimili, kwenye mambo mbalimbali.*

*Kukokotoa hesabu, Doto kwake ni urojo,*
*Uchafu kwake ni tabu, mazingira yupo chonjo,*
*Masomo yote nakiri, Amina ndiye kionjo,*
*Amina yeye hapendi, ushirika wa makundi.*

*Kusoma ndani ya kundi, Amina kwake si hoja,*
*Amepunguza ushindi, ameukosa umoja,*
*Alijiona mshindi, upweke hauna tija,*
*Amina yeye hapendi, ushirika wa makundi.*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5

1. Umejifunza nini katika shairi hili?
2. Ni mafanikio gani waliyonayo marafiki watatu uliowasoma katika shairi hili?
3. Taja hasara ambazo amezipata Amina baada ya kushindwa kushirikiana na wenzake shuleni.
4. Je, utamshauri nini mwenzako ambaye hapendi kushirikiana na wenzake?

## Zoezi la 6

1. Je, ni shughuli zipi za kujitolea unazoweza kushiriki katika eneo unaloishi?
2. Ni rasilimali zipi zinazopatikana katika eneo unaloishi?
3. Andika wajibu ulionao katika familia yako.

## Zoezi la 7

Chagua jibu sahihi kisha andika herufi yake katika kisanduku.

1. Matendo ya uwajibikaji katika familia ni pamoja na:
   (a) kulala mapema
   (b) kushiriki kufanya kazi ndogondogo za familia
   (c) kucheza mpira
   (d) kuwatibu wagonjwa ☐
2. Shughuli za usafi nyumbani zinapaswa kufanywa na:
   (a) baba
   (b) mama
   (c) msaidizi wa nyumbani
   (d) wanafamilia wote ☐

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Baadhi ya shughuli za kujitolea katika jamii ni pamoja na:
   (a) kumwagilia bustani ya familia
   (b) kufanya usafi katika zahanati ya kijiji au mtaa
   (c) kudeki chumba chako cha kulala
   (d) kulisha mifugo ya familia

4. Ni matendo yapi kati ya haya yanaonesha kuthamini rasilimali za jamii?
   (a) Kutoboa bomba la maji ili kuchota maji ya kumwagilia bustani
   (b) Kupanda miti kandokando ya vyanzo vya maji
   (c) Kulisha mifugo katika misitu ya hifadhi
   (d) Kuchoma moto msitu ili kurina asali

## Msamiati

| | |
|---|---|
| **Kitovu** | chanzo cha kitu au jambo |
| **Kunufaika** | kupata manufaa |
| **Kuwajibika** | kutimiza au kutekeleza jambo linalokulazimu kulifanya |
| **Pembezoni** | pembeni mwa |
| **Takribani** | yapata au karibia |
| **Uzalendo** | kuipenda nchi na kuwajibika kwa ajili ya nchi yako |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Saba

## Kutii sheria na kanuni

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza kutambua sheria na kanuni za shule. Pamoja na hayo, utajifunza kuepuka vitendo vya ukiukwaji wa sheria na kanuni mbalimbali. Pia, utajifunza utekelezaji wa majukumu ya kila siku kwa kuzingatia kanuni na taratibu za familia. Umahiri utakaoupata katika sura hii utakuwezesha kuwa na ufanisi katika shughuli zako za kila siku.*

### Kutii sheria

Sheria ni utaratibu wa kufuatwa katika kutekeleza jambo. Kutii sheria ni kufuata kanuni na utaratibu uliowekwa kwenye maeneo mbalimbali. Ni vyema ukatambua kuwa, ni muhimu kufuata sheria zilizowekwa shuleni. Baadhi ya sheria hizo ni kuwahi shuleni na kuhudhuria masomo. Aidha, unapaswa kuvaa sare za shule, kuheshimu viongozi na kutopigana shuleni.

*Tazama picha hizi, kisha jibu maswali.*

1.



FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2.



3.



**Kielelezo namba 1:** *Wanafunzi wakionyesha matendo ya kutii sheria za shule.*

**Zoezi la 1**

1. Unaona nini katika picha 1, 2 na 3?
2. Matendo gani zaidi ya unayoyaona katika picha yanaonesha kutii sheria za shule?
3. Wanafunzi wasiofuata sheria za shule wanafanywa nini?
4. Ni sheria zipi za shule yako unazozifahamu?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Andika hatua utakazochukua kumsaidia rafiki yako asiyetii sheria za shule.

## Kubaini faida za kutii sheria za shule

*Soma mazungumzo haya, kisha jibu maswali.*

**Hamisi:** Habari, Neema?

**Nesema:** Nzuri tu.

**Hamisi:** Eti Neema, kwa nini wewe unafaulu vizuri sana mitihani yako?

**Neema:** Mimi nawahi shuleni, nahudhuria vipindi, nazingatia masomo na kuheshimu walimu.

**Hamisi:** Ahaaa! Je, unafikiri mimi nikifanya hayo nitafaulu kama wewe?

**Neema:** Ni kweli kabisa, mambo hayo yatakusaidia kujifunza vizuri.

**Hamisi:** Asante kwa maelezo yako. Nami nitazingatia ushauri wako.

**Zoezi la 2**

1. Je, kuna faida gani za kuwahi shuleni?
2. Ni sababu gani zinazomfanya Neema afaulu vizuri?
3. Kuna faida gani za kutii sheria na kanuni za shule?
4. Unapata hasara gani usipotii sheria na kanuni za shule?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kujenga nidhamu binafsi

Nidhamu binafsi ni kufanya mambo yanayofaa kwa kujipangia mwenyewe. Matendo yanayoonesha nidhamu binafsi ni kama vile kufanya kazi kwa wakati. Aidha, unapaswa kuweka ratiba ya kujisomea, kuifuata na kujituma katika kufanya kazi. Pia kutumia muda vizuri na kupangilia kazi ni sehemu ya nidhamu binafsi.

*Chunguza vitendo hivi, kisha jibu maswali.*

(a) Mwanafunzi amekamilisha kazi alizopewa na mwalimu kwa wakati.

(b) Mwanafunzi ameweka utaratibu wa kujisomea nyumbani na kuufuata.

(c) Mwanafunzi anajitolea kufuta ubao kabla ya mwalimu kuanza kufundisha.

(d) Mwanafunzi anasafisha eneo lake kabla ya kuingia darasani.

(e) Mwanafunzi anakuwa nadhifu muda wote.

(f) Mwanafunzi anafanya usafi nyumbani kabla ya kwenda shuleni.

**Zoezi la 3**

1. Je, unajifunza nini kutokana na vitendo hivyo?
2. Je, wewe unaweza kutenda vitendo gani kati ya hivyo?
3. Tabia kama hizi zina faida gani?
4. Ni vitendo gani vingine utakavyofanya shuleni na nyumbani ili kujijengea nidhamu binafsi?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Soma habari hii, kisha jibu maswali.*

Mongi na Salumu ni marafiki wanaosoma Shule ya Msingi Maendeleo. Wanaporudi nyumbani kutoka shule, Mongi hufanya kazi zake kwa kufuata ratiba aliyojiwekea. Kazi hizo ni kumwagilia bustani na kufua nguo zake za shule. Vilevile, hufanya mazoezi aliyopewa shuleni. Salumu hafanyi kazi hadi akumbushwe na kusimamiwa na mama yake.

**Zoezi la 4**

1. Ni matendo gani ya kujituma yanayooneshwa na Mongi?
2. Ni matendo gani ya kujituma utakayotenda baada ya kujifunza sehemu hii?
3. Nini madhara ya kutojituma?

**Kazi ya kufanya**

1. Tengeneza ratiba binafsi ya kujisomea na uone kama unaweza kuifuata.
2. Kama unaweza eleza kwanini unaweza na kama hujaweza eleza kwanini hujaweza.
3. Tengeneza ratiba binafsi ya kazi za shuleni na nyumbani.

## Kujituma katika kazi

*Soma habari hii, kisha jibu maswali.*

Hanga ni mwanafunzi wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Pamba. Yeye hutii sheria za shule na maagizo ya wazazi. Anapoamka huwasalimia watu wote nyumbani, hufanya usafi wa chumba chake na kuosha vyombo. Kisha, huenda shuleni.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Anapokuwa shuleni hufanya kazi anazopewa na hujitolea kufanya kazi zingine. Siku moja mwalimu mkuu alimwona Hanga akimwagilia bustani ya maua. Alimuuliza iwapo kuna mwalimu ambaye alimtuma kufanya hivyo. Hanga alisema aliamua kufanya bila kuagizwa. Wakiwa mstarini mwalimu mkuu alimwita Hanga na kumpa zawadi mbele ya wanafunzi.

**Zoezi la 5**

1. Neno kujituma lina maana gani?
2. Ni matendo gani ya kujituma aliyofanya Hanga uliyojifunza kutoka katika habari hii?
3. Ni matendo gani ya kujituma utakayotenda baada ya kusoma habari hii?

**Kazi ya kufanya**

1. Andika matendo matatu ambayo umewahi kujituma katika maisha yako.
2. Andika faida ulizozipata kwa kujituma huko.

## Kupenda Kujisomea

Kupenda kujisomea ni sehemu ya matendo yanayoonesha nidhamu binafsi. Utapata faida kubwa kwa kupenda kujisomea. Mtu anayependa kujisomea huwa na nidhamu katika kutafuta maarifa. Huzingatia ratiba yake ya kujisomea na hufuata utaratibu aliojiwekea. Mtu anayependa kujisomea huongeza maarifa kila siku.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Soma mazungumzo haya, kisha jibu maswali.*

| | |
|---|---|
| **Siwema:** | Shikamoo, mwalimu. |
| **Mwalimu:** | Marahaba Siwema. Hujambo? |
| **Siwema:** | Sijambo, mwalimu. |
| **Mwalimu:** | Nikusaidie nini, Siwema? |
| **Siwema:** | Samahani mwalimu, naomba msaada wako. |
| **Mwalimu:** | Msaada gani? |
| **Siwema:** | Mwalimu, muhula uliopita sikufanya vizuri kwenye masomo yangu. |
| **Mwalimu:** | Pole sana. Unapaswa kuongeza bidii katika kujisomea. |
| **Siwema:** | Mwalimu, nitafanyaje ili niweze kujenga tabia ya kujisomea? |
| **Mwalimu:** | Tengeneza ratiba yako binafsi ya kujisomea na uizingatie. |
| **Siwema:** | Nimekuelewa mwalimu. Sikuwa na ratiba binafsi ya kujisomea. Nitakwenda kuiandaa. |
| **Mwalimu:** | Ukijenga tabia ya kujisomea utafanya vizuri kwenye masomo na utafaulu mitihani yako. |
| **Siwema:** | Asante sana mwalimu. |
| **Mwalimu:** | Usisite kuja kuomba msaada muda wowote. |
| **Siwema:** | Kwa heri mwalimu. |
| **Mwalimu:** | Kwa heri Siwema. |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 6**

1. Je, ni ushauri gani aliotoa mwalimu kwa Siwema?
2. Ni mambo gani mengine yatakayokufanya upende kujisomea?
3. Utapata faida gani ukipenda kujisomea kama Siwema?

## Kuepuka kuvunja sheria na kanuni

Mwanafunzi, ni vyema kutii sheria na kanuni zinazokuongoza katika maisha ya kila siku. Je, unatii sheria na kanuni za shule? Ni muhimu kutii sheria na kanuni za shule ili uweze kujifunza vizuri masomo yako.

*Hebu tafakari matendo yafuatayo:*

1. Mtoto anatupa takataka barabarani.
2. Mwanafunzi anajisaidia kichakani.
3. Kijana anachimba mfereji ili maji machafu yatiririke kwenye mto.

Je, nini madhara ya matendo haya? Matendo yapi kati ya haya hufanyika katika mazingira unayoishi? Je, utatoa ushauri gani kwa watu wenye tabia kama hizi?

Sheria ni muhimu katika jamii yoyote. Wanajamii huishi kwa amani ikiwa kuna utii wa sheria na kanuni zinazowaongoza. Ukiukwaji wa sheria na kanuni una madhara katika jamii. Madhara hayo ni pamoja na vifo, milipuko ya magonjwa, na migogoro.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kusimamia utekelezaji wa sheria na kanuni shuleni

Ili kuhakikisha utii wa sheria ni muhimu kuwa na usimamizi bora wa sheria hizo.

Je, utachukua hatua gani ukiona matendo yafuatayo?

1. Mwanafunzi mwenzako akivuta bangi.
2. Mwanafunzi mwenzako akiruka ukuta na kutoroka shuleni.
3. Wanafunzi wakijisaidia haja ovyo kwenye eneo la shule.
4. Wanafunzi wakimpiga mwanafunzi mwenzao.

*Soma shairi hili, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Zakaria na Mgisa, viranja shule Mivinje,
Husimamia kabisa, kanuni zisitupwe nje,
Zakaria ndiye hasa, wa usafi ndani na nje,
Kutekeleza kanuni, lazima kusimamiwe.

Mgisa Kiranja Mkuu, maagizo hupokea,
Mwalimu wake wa zamu, utaratibu hutoa,
Naye hutia muhimu, kazi kuzisimamia,
Kutekeleza kanuni, lazima kusimamiwe.

Viongozi wa darasa, usafi kusimamia,
Ndani ya lake darasa, utulivu simamia,
Walimu nao ruhusa, vipindi jifundishia,
Kutekeleza kanuni, lazima kusimamiwe.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mwalimu aliye zamu, taarifa hupokea,
Viranja walio zamu, wajibu tekelezea,
Hili jambo ni muhimu, kanuni kusimamia,
Kutekeleza kanuni, lazima kusimamiwe.

**Zoezi la 7**

1. Je, ni majukumu yapi anayofanya Zakaria ambayo hufanyika pia shuleni kwenu?
2. Taja shughuli ambazo unaweza kuzisimamia na kuzitekeleza ukiwa nyumbani.
3. Je, ukipata nafasi ya Mgisa, ni mambo gani utaweza kuyasimamia shuleni kwenu?
4. Licha ya kufundisha, walimu wako husimamia mambo gani mengine shuleni?

Bila shaka umetambua umuhimu wa kusimamia utekelezaji wa sheria na kanuni shuleni. Hivyo, unatakiwa uwe mfano wa kuigwa katika kufuata sheria na kanuni. Pia uwaelimishe wanafunzi wenzako kufuata sheria na kanuni za shule. Vilevile, unao wajibu wa kuchukua hatua unapobaini vitendo vinavyokiuka sheria na kanuni za shule.

**Kazi ya kufanya**

Orodhesha matendo yanayoonesha utii wa sheria za shule. Andika matendo hayo katika daftari lako.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 8

1. Orodhesha faida tatu anazoweza kuzipata mtu anayependa kujisomea.
2. Andika faida tatu za kusimamia sheria na kanuni za shule.
3. Orodhesha njia mbili za kuwasaidia wenzako wajenge tabia ya kutii sheria na kanuni.

## Kazi ya kufanya

Andika hatua utakazochukua kumsaidia rafiki yako asiyetii sheria za shule.

## Msamiati

**Kanuni** taratibu zinazotumika mahali fulani

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nane

## Kuwa mvumilivu

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza kuvumilia na kustahimili changamoto zinazokukabili. Vilevile, utajifunza kukubali kukosolewa na kutatua changamoto unazokutana nazo katika mazingira yako kwa kutumia mbinu mbalimbali. Umahiri utakaoupata katika sura hii utakuwezesha kutatua changamoto mbalimbali utakazokumbana nazo katika mazingira yako kwa kutumia njia sahihi na lugha yenye staha.*

### Kukubali changamoto

Changamoto ni kitu au jambo ambalo humkwamisha mtu kufikia lengo alilojiwekea. Unatakiwa kuwa mstahimilivu unapopata changamoto. Pia, unatakiwa kuikubali na kutafuta namna ya kukabiliana nayo. Unapopata changamoto, unashauriwa usitende matendo ya kujidhuru. Aidha, unaposhindwa kupata njia ya kukabiliana na changamoto ni vyema ukaomba ushauri kwa watu, au kutumia uzoefu wa watu wengine.

Je, umewahi kupata changamoto? Ulichukua hatua gani kuikabili changamoto hiyo?

*Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Zuma na Janeti walikuwa wanaishi maisha ya raha. Baba yao alikuwa meneja katika kampuni kubwa huko Dar es Salaam. Mama yao hubaki nyumbani kwa ajili ya kulea watoto. Kwao kulikuwa na wasaidizi wanne wa kazi za nyumbani. Kila mwisho wa juma walipelekwa ufukweni na maeneo ya kuchezea watoto. Kila siku walipelekwa shuleni kwa gari. Wakati wa likizo

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

wazazi wao waliwapeleka kwenye mbuga za wanyama. Siku moja ilitangazwa kuwa kampuni aliyokuwa akifanyia kazi baba yao imefilisiwa. Wafanyakazi wote walipoteza ajira zao. Kipato cha familia kilishuka. Safari za kwenda ufukweni na sehemu za michezo hazikuwepo tena. Hawakula vizuri tena kama ilivyokuwa mwanzo.

Zuma na Janeti walienda shuleni na kurudi kwa miguu. Baada ya siku mbili walishindwa kwenda shule kwa kuwa walichoka. Siku iliyofuata, baba yao aliwasimulia kisa cha kweli kinachohusu maisha yake ya utotoni. Alifanya hivyo ili kuwajengea ustahimilivu. Aliwaeleza kuwa, yeye alitembea kilometa kumi wakati wa kwenda shule na kurudi nyumbani. Alitembea umbali huo kila siku kwa muda wa miaka saba. Licha ya vikwazo hivyo, alifanikiwa kufaulu mitihani yake na kusoma hadi elimu ya juu. Zuma na Janeti walihamasika na kisa cha maisha ya baba yao. Wakaamua kufanya bidii nyumbani na shuleni.

FOR ONLINE USE ONLY

**Zoezi la 1**

1. Kisa cha Zuma na Janeti kinakufundisha nini?
2. Ni tabia gani iliyomsaidia baba yake Zuma kufaulu vizuri mitihani yake?
3. Nini kingetokea iwapo Zuma na Janeti wasingebadilika?
4. Utamsaidiaje mwenzako mwenye changamoto kama hizi?

**Kazi ya kufanya**

Eleza changamoto kubwa uliyowahi kukutana nayo na jinsi ulivyoikabili.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kutatua changamoto

Bila shaka umejifunza umuhimu wa kukubali changamoto zinazokukabili. Unapokubali changamoto unajenga uwezo wa kuzikabili. Yakupasa kuwa makini ili kupata ufumbuzi wa changamoto zinazokukabili.

*Soma kisa hiki, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Zubeda na Herida ni watoto pacha wa Mzee Heri na Bi. Paulina. Walikuwa ni watoto wa pekee kwa wazazi wao. Walipewa mahitaji yao yote, na waliishi maisha ya raha sana. Siku moja Mzee Heri alipatwa na homa kali. Alikimbizwa hospitalini lakini baada ya siku tatu alifariki. Yalikuwa majonzi makubwa sana kwa familia yao. Kama ilivyo desturi, watu wengi walikuja kwenye msiba. Msiba ulipoisha, kila mtu aliondoka na kuwaacha Bi. Paulina na wanawe. Baada ya muda mfupi hali ya nyumbani ilibadilika. Watoto walikosa mahitaji muhimu. Hali iliyomsababishia Zubeda kuwa ombaomba mtaani ili apate fedha za nauli na kununua sare za shule. Mama yake alimuonya lakini hakusikia.

Kwa upande wa Herida yeye hakujihusisha na vitendo vya kuombaomba. Alistahimili hali ngumu ya maisha. Alikubali kuvaa viatu jozi moja na kutembea kwa miguu kwenda shuleni. Alijiwekea malengo katika maisha yake ya baadaye. Aliomba ushauri kwa mwalimu wa darasa, wajomba zake na marafiki wa baba yake. Pia, aliongea na wenzake na watu wazima waliopitia kwenye changamoto kama yake. Baadhi walimshauri aanze biashara ndogondogo. Wengine walimshauri atenge saa za kusoma na nyingine za kumsaidia mama yake. Herida alishirikiana na mama yake kuanzisha shughuli ndogondogo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Walianza kulima bustani za mboga na kuzisambaza kwa wateja mbalimbali. Kila siku baada ya kutoka shuleni, Herida alishughulikia bustani za mboga na baada ya hapo alijisomea. Siku za mwisho wa juma alimsaidia mama yake kusambaza mboga kwa wateja. Bi. Paulina aliweza kupata fedha za kuikimu familia.

Herida hakutetereka kabisa kwenye masomo yake. Aliendelea kufanya vizuri darasani. Hata hivyo, alimweleza mwalimu wa malezi na unasihi juu ya tabia ya dada yake. Mwalimu alimkanya Zubeda na hatimaye aliachana na kuombaomba mtaani. Wote kwa pamoja walisoma kwa bidii. Hatimaye waliweza kuendelea na masomo hadi chuo kikuu. Sasa hivi Herida ni mwalimu na Zubeda ni daktari bingwa wa watoto.

**Zoezi la 2**

1. Ni tabia ipi iliyooneshwa na Herida kwenye kisa hiki?
2. Je, nini kingetokea endapo Zubeda na Herida wangeshindwa kutatua changamoto zilizowakabili?
3. Taja matukio mengine kama haya uliyowahi kukutana nayo.
4. Utamsaidiaje mwenzako aliyeshindwa kuzikabili changamoto?
5. Je, utafanya nini kutatua changamoto ulizonazo?

**Kazi ya kufanya**

Chunguza wanafunzi wa darasa lako, kisha, orodhesha changamoto zao tatu za kimaisha. Andika ushauri unaoweza kutoa kuhusu changamoto hizo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Soma kisa kingine kuhusu wanafunzi wawili, Keto na Joshi.*

Keto na Joshi walikuwa marafiki wakubwa. Lakini walikuwa na tabia tofauti. Keto akipata changamoto ya aina yoyote anakuwa msiri. Hamwambii mtu yeyote. Joshi akipata changamoto yoyote hata iwe ndogo kiasi gani, lazima amwambie Keto.

Keto alikuwa hodari sana wa somo la English lakini dhaifu kwenye Hisabati. Joshi alikuwa bingwa wa somo la Hisabati lakini dhaifu kwenye somo la English. Kila wanapofanya jaribio, Joshi huenda kwa Keto kumuonesha alama zake na kuomba msaada. Joshi alikuwa haishii hapo. Alienda kwa wanafunzi wa madarasa mengine na hata kwa walimu wake kuomba msaada. Lakini Keto alipopata alama ndogo kwenye Hisabati aliificha na kusononeka mwenyewe moyoni. Hakumwambia mtu yeyote wala kuomba msaada wowote.

Wanafunzi wenzake walidhani kuwa yeye alikuwa bingwa wa masomo yote. Kwenye matokeo yake ya mtihani wa mwisho, Keto hakufanya vizuri katika somo la Hisabati. Rafiki yake Joshi alifaulu vizuri sana kwenye masomo yote. Wanafunzi wote walimshangaa Keto kwani hawakutegemea.

**Zoezi la 3**

1. Taja tabia za Keto na Joshi zinazooneshwa kwenye kisa hicho.
2. Je, ni tabia zipi nyingine zinazofanana na hizo unazozifahamu?
3. Je, Keto alikuwa na changamoto gani?
4. Je, wewe ungetoa ushauri gani kwa Keto?
5. Joshi alifanya nini kutatua changamoto zake?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Andika mambo utakayofanya katika maisha yako kutokana na ulichojifunza kwenye kisa hiki. Andika kazi yako nyuma ya daftari.

## Kukubali kukosolewa

Hakuna mtu asiyekosea. Wote tunaimarishwa na jamii inayotuzunguka kwa njia ya kutukosoa pale tunapokosea. Anayekupenda atakukosoa. Asiyekupenda atakuacha ubaki na tatizo. Kukubali kukosolewa ni jambo la hekima sana.

Je, unaposahihishwa na mwenzako huwa unafanyaje? Kuna faida zipi za kukubali kukosolewa?

*Soma majigambo yafuatayo, kisha jibu maswali.*

**Juma**: Mimi ni hodari sana kwenye mchezo wa mpira. Nisipokwenda mpirani mchezo hauanzi.

**Jumanne**: La hasha! Mimi ninakuzidi. Kwenye mpira hunipati. Mimi ndiye mchezaji bora hapa shuleni.

**Jonathan**: Lakini nyie watu, mbona hamna habari na masomo? Mnashughulikia mpira tu.

**Juma**: Kwani michezo haina maana yoyote?

**Jonathan**: Sisemi hivyo, lakini naona hamna umakini wowote kwenye masomo kama mnaouonesha kwenye michezo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Jumanne**: Juma inabidi tukubali kukosolewa pale tunapofanya makosa. Ni kweli michezo ni mizuri, lakini tunakosea kwa kutofanya juhudi kwenye masomo.

**Joshua**: Achana na mambo ya masomo, mimi na mpira tu. Michezo kwangu ni muhimu kuliko masomo.

**Jonathan**: Hata mimi nilikuwa hodari sana kwenye mpira. Lakini ni vyema masomo uyape nafasi. Niliona kuwa nafanya makosa na nilikubali kukosolewa. Sasa hivi nimeyapa masomo nafasi yake. Ninafanya vizuri kwenye masomo yangu, tofauti na siku za nyuma. Lakini wenzangu mmebaki palepale.

## Zoezi la 4

1. Je, ni matendo gani ya kukubali kukosolewa yanayotajwa kwenye majigambo?
2. Unafikiri wanafunzi hao wanaweza kupata matatizo gani kwa kukataa kukosolewa?
3. Je, ungekuwa Jumanne ungewashauri nini zaidi wenzako?
4. Je, ukiwa na rafiki yako mwenye tabia kama ya Juma utamshauri nini?

FOR ONLINE USE ONLY

## Kazi ya kufanya

Soma magazeti mbalimbali. Bainisha habari au kisa kinacho onesha matendo ya mtu asiyekubali kukosolewa. Weka kipande cha gazeti hilo nyuma ya daftari lako.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5

Oanisha maneno ya **sehemu A** na yale yaliyoko **sehemu B** ili kupata maana sahihi.

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| i. Kukosoa | (a) Kukubali kosa na kuomba radhi |
| ii. Kushauri | (b) Kueleza mapungufu au makosa ya mtu mwingine |
| iii. Kusikiliza mawazo ya wengine | (c) Kutoa maelekezo jinsi ya kutatua tatizo |
| iv. Kuomba msamaha | (d) Kuwatoroka watu wanaokupinga |
| | (e) Kujitahidi kuelewa mawazo ya wengine na kuyafuata |
| | (f) Kupiga kelele watu wanapokupinga |

## Msamiati

**Changamoto** kitu au jambo linaloweza kukwamisha kufikia lengo ulilojiwekea

**Kufilisika** kuishiwa mali

**Ustahimilivu** hali ya kufanya jambo kwa uvumilivu

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tisa

## Kufikia malengo

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza vitendo vinavyoashiria mtazamo chanya na fikra za kujitegemea. Pia, utajifunza kudadisi mambo, kuishi kwa malengo na njia za kutatua matatizo ili kufikia malengo. Umahiri utakaoupata katika sura hii utakuwezesha kuishi kwa amani katika mazingira yako, pia kushiriki vema katika shughuli mbalimbali za ujenzi wa jamii yako kwa ustahimilivu.*

### Mtazamo chanya

Mwanafunzi ni vyema kujiamini kwamba unao uwezo wa kufanya mambo kwa mafanikio. Imani ya kwamba unaweza kufaulu masomo, kukamilisha kazi na kuhitimu elimu msingi huitwa mtazamo chanya. Mtazamo chanya hukusaidia kufikia malengo, kupata mafanikio na kuishi vizuri. Pia, mtazamo chanya hukupa matarajio ya kufanikiwa katika jambo. Je, unatarajia nini katika maisha yako?

Utawezaje kujenga tabia ya mtazamo chanya? Utapata faida gani kwa kuwa na mtazamo chanya? Ufanye nini ili kuonesha kuwa una mtazamo chanya?

*Soma kisa hiki, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Maria na Tina ni marafiki wawili waliokuwa wakisoma Shule ya Msingi Ramo. Wote wawili walikuwa wakifanya vibaya sana kwenye masomo yao. Kila wakijitahidi kusoma waliendelea kushindwa mitihani. Maria hakukata tamaa. Aliamini kuwa atapata ufumbuzi wa tatizo lake na kufanikiwa kwenye

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

masomo yake. Alifanya bidii kufikia lengo hilo. Kwa kutumia ubunifu aliwashawishi wenzake kuunda kikundi cha kujisomea. Aliwashirikisha wanafunzi wenye uwezo kwenye masomo mbalimbali. *Je, unafikiri ni kwa nini alifanya hivyo?* Hii ilisaidia kikundi chao kuwa na wanafunzi wenye uwezo mzuri katika kila somo. Walikubaliana kuwa kila mwanafunzi amuombe mwalimu wa somo analofanya vizuri kumwandalia maswali ya ziada. Kila mwisho wa juma wote waliamka mapema na walifanya shughuli zote walizopangiwa. Kila ilipotimu saa tano asubuhi walikutana nyumbani kwa kina Maria na kusoma pamoja. Walihakikisha kuwa wanajibu maswali yote yaliyo andaliwa na walimu wao. Baadaye kila mmoja wao alipeleka kazi kwa mwalimu wake kwa masahihisho. Baada ya miezi sita, Maria aliongoza kimasomo darasani. Wanafunzi wenzake walishangazwa na kufurahishwa na jambo hilo.

**Zoezi la 1**

1. Je, tabia iliyooneshwa na Maria inakufundisha nini?
2. Baada ya kusoma kisa hiki utamsaidiaje mwenzako asiyependa kusoma?
3. Taja hatua ambazo ungechukua kukabiliana na changamoto kama alizopata Maria.
4. Je, unafikiri kuna faida gani nyingine za kuwa na mtazamo chanya?

**Kazi ya kufanya**

Zungumza na mwalimu wa somo akusimulie alivyofanikiwa kwa kuwa na mtazamo chanya. Andika maelezo katika ukurasa wa nyuma ya daftari lako.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kujifunza kwa njia ya makundi

Wanafunzi wakiwa shuleni hutarajia kufanya vizuri katika mitihani yao. Katika sehemu hii tutajifunza jinsi ya kutumia makundi katika kujifunza.

Je, makundi ya kujifunza yana manufaa gani? Ili makundi hayo yawe na manufaa yanatakiwa yaweje? Ni mambo gani ya kuzingatia katika kujifunza kwa makundi?

Makundi yanamjenga mtu. Kwa mfano, unapojifunza kwa kutumia makundi unatumia uzoefu na uelewa wa watu wengi. Vipaji hutofautiana, hivyo unapokuwa katika makundi unafaidi vipaji vya wanafunzi wenzako. Pia, wewe unapata uwezo wa kutoa uzoefu wako kwa wenzako. Hivyo unapata nafasi ya kukuza kipaji chako.

*Angalia picha hizi, kisha jibu maswali yanayofuata.*

1.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2.




**Kielelezo namba 1:** *Kujifunza kwa njia ya makundi*

## Zoezi la 2

1. Ni tendo gani unaliona kwenye picha namba moja?
2. Je, ni matendo gani kati ya hayo hufanyika shuleni kwenu?
3. Kuna faida gani ya kushirikiana katika kufanya mambo mbalimbali?
4. Utawashauri nini wenzako ili wawe na tabia ya kushirikiana kutenda mambo mbalimbali?

*Soma kisa kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Sudi na Jonatha ni marafiki wakubwa. Walikuwa hawafanyi vizuri kwenye masomo. Kila mmoja alikuwa akijisomea peke yake. Baada ya kutafakari, waliamua kubadili namna yao ya kujifunza. Waliunda kikundi cha kusoma pamoja. Walizingatia masomo waliyokuwa hawafanyi vizuri ili waweze kujifunza kwenye kikundi. Waliwashawishi wanafunzi wenye uwezo mkubwa kwenye masomo hayo kujiunga kwenye kikundi chao.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Waliunda kanuni za kuendesha kikundi chao pamoja na ratiba ya kujisomea. Walikubaliana kukutana shuleni kila Jumamosi kwa lengo la kujisomea. Kila mwanakikundi alishiriki katika kuwaelekeza wenzake mambo aliyokuwa anayafahamu. Sudi na Jonatha walihakikisha kuwa kila wanapopewa jukumu wanalitekeleza kikamilifu. Ikiwa jukumu liko nje ya uwezo wao, walitafuta watu wa kuwasaidia. Baada ya kubadili namna ya kujifunza, Sudi na Jonatha walifanya vizuri katika masomo yote.

**Zoezi la 3**

1. Je, ni mbinu zipi za kutatua tatizo walizozitumia Sudi na Jonatha?
2. Unafikiri kwa nini waliunda kanuni za kikundi?
3. Ni faida zipi nyingine za kusoma kwa makundi?
4. Je, ni mambo gani mengine unayoweza kufanikiwa kwa njia ya makundi?

**Kazi ya kufanya**

Jadiliana na wenzako kuhusu makundi ya kujifunza yaliyopo shuleni. Ainisha faida za makundi hayo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kujitegemea katika maisha

Bila shaka umewahi kutatua matatizo au kufanya maamuzi sahihi bila kushawishiwa na mtu mwingine. Hii ni pamoja na kukataa kushawishiwa kufanya matendo yasiyofaa. Matendo hayo yanajumuisha kutoroka shuleni, kupigana, na kutumia lugha isiyofaa. Aidha, kuacha kufanya kazi za darasani ni tendo lisilofaa pia. Uwezo wa kutatua matatizo au kufanya maamuzi sahihi peke yako ndiyo huitwa kujitegemea.

Unapaswa kutumia vipaji na uwezo ulionao kutenda matendo ya kujitegemea. Matendo hayo ni kama vile kufua nguo zako na kusafisha chumba chako. Vilevile, unapaswa kujitegemea na kupanga ratiba ya kujisomea wewe mwenyewe.

Umeshawahi kufanya maamuzi wewe mwenyewe bila ya kumtegemea mtu mwingine? Je, unachukua hatua gani kwa somo unalofanya vibaya?

*Tafakari matendo yafuatayo:*

1. Mwanafunzi anasoma kwa bidii ili aweze kufaulu masomo yake.
2. Mwanafunzi amegundua mbinu mpya za kujifunza.
3. Mwanafunzi wa darasa la tano anagombea nafasi ya kiranja mkuu wa shule.
4. Mwanafunzi wa darasa la kwanza anafua nguo zake mwenyewe.

Je, umegundua nini kutokana na matendo haya? Bila shaka utakuwa umetambua kuwa matendo hayo huonesha stadi za kujitegemea. Ni vizuri kuwa na fikra za kujitegemea katika maisha yako.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Soma kisa kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Mwasi na Tausi ni watoto wa Mzee Salumu. Wanasoma Shule ya Msingi Goweko. Tausi anasoma darasa la nne na dada yake Mwasi anasoma darasa la sita. Watoto hawa wana juhudi katika masomo yao. Hutafuta mbinu mbalimbali za kuwasaidia kuweza kujifunza. Tausi hupenda somo la Hisabati wakati Mwasi hupenda somo la Maarifa ya Jamii.

Tausi ametengeneza orodha ya namba kwa kutumia makasha na kuibandika kwenye ukuta wa darasa. Hutumia orodha hiyo ya namba kujifunza na wenzake. Mwasi ameweza kutengeneza kifani cha tufe la dunia kwa kutumia udongo wa mfinyanzi. Alikipaka rangi kifani hicho na kukiweka kwenye ofisi ya walimu. Wote wawili ni jasiri, mara nyingi hufanya maamuzi yao wao wenyewe. Pia wameanzisha kikundi cha kujisomea ili kusaidiana kwenye masomo kila mwisho wa juma. Wanafanya vizuri sana kwenye masomo yao. Vilevile, Tausi ni kiranja katika darasa lake, na Mwasi ni kiranja mkuu wa shule. Mwasi aliwahi kugombea nafasi ya kiranja mkuu alipokuwa darasa la tano. Wanafunzi wenzake waliona ni jukumu kubwa kwake lakini yeye alijiamini kuwa angeweza. Hata hivyo, alikosa nafasi hiyo hadi uchaguzi uliofuata. Sasa hivi ndiye kiranja mkuu wa shule na ni kiongozi mzuri sana.

Wakiwa nyumbani hushiriki katika miradi ya familia. Tausi hushiriki kupanga bajeti ya vyakula vya kuku. Mwasi yeye huwahudumia wateja wanaokuja kununua kuku na mayai. Wamejifunza kiasi cha kutosha njia za ufugaji wa kuku. Ndoto yao ni kujishughulisha na shughuli za ufugaji baada ya kumaliza shule.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 4**

1. Matendo yanayoonekana kwenye kisa hiki yanaashiria nini?
2. Ni stadi zipi za kujitegemea unazoziona kwenye kisa hiki?
3. Je, wewe umewahi kujenga stadi zipi kati ya hizo?
4. Taja mambo unayofanya bila kusaidiwa na mwalimu, mzazi au mlezi.

**Kazi ya kufanya**

Orodhesha mambo unayopaswa kufanya peke yako bila mwongozo. Andika mambo hayo kwenye kurasa za nyuma za daftari lako.

FOR ONLINE USE ONLY

## Kudadisi mambo mbalimbali

Ili uweze kujifunza vyema, unapaswa kuwa na tabia ya kudadisi mambo mbalimbali.

Je, una tabia ya kudadisi mambo? Uliwahi kudadisi mambo gani?

*Soma mazungumzo haya, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Kitila**: Habari ya asubuhi kaka Msechu.

**Msechu**: Salama.

**Kitila**: Kaka, naomba nikuulize jambo.

**Msechu**: Uliza tu mdogo wangu.

**Kitila**: Kwa nini nchi yetu ni maskini? Inawezekanaje tuwe maskini wakati tuna madini, bahari, mbuga za wanyama, ardhi yenye rutuba na gesi?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Msechu**: Kuwa na rasilimali siyo kigezo cha nchi kuwa tajiri.

**Kitila**: Nini kinasababisha tuwe maskini sasa?

**Msechu**: Uwezo mdogo wa kutumia rasilimali katika uzalishaji.

**Kitila**: Sawa, lakini kwani ni lazima tuzalishe? Hatuwezi kuuza rasilimali hizo?

**Msechu**: Ni kweli, tunaweza kuziuza, lakini tutaziuza kwa thamani ndogo wakati tukitengeneza vitu vinakuwa na thamani kubwa. Kwa mfano; pamba huuzwa kwa pesa kidogo kuliko shati linalotokana na pamba.

**Kitila**: Ahaa! Sasa nimekuelewa. Kwani haya maarifa unayapataje?

**Msechu**: Vipo vyanzo vingi vya taarifa sahihi. Vyanzo hivi ni vitabu, magazeti, majarida, wataalamu na mitandao ya mawasiliano. Mimi hudadisi mambo mengi kutoka katika vyanzo hivyo.

**Zoezi la 5**

1. Ni tabia zipi zinazokuvutia kuhusu Kitila na Msechu?
2. Je, Kitila amenufaika vipi kutokana na udadisi?
3. Ni faida gani zingine unazoweza kupata kwa kuwa mdadisi?

**Kazi ya kufanya**

Chunguza matendo ya udadisi yanayofanywa na wanafunzi wenzako. Kati ya matendo hayo orodhesha matendo ya udadisi ambayo ungependa kuyafanya.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kujiwekea malengo

Katika sehemu iliyopita umejifunza kuwa mdadisi kuhusu mambo mbalimbali. Sasa utajifunza jinsi ya kujiwekea malengo na namna ya kuyafikia. *Je, una malengo gani kuhusu masomo yako? Je, ungependa kuwa nani utakapomaliza shule? Je, utafanya nini kufikia malengo hayo?*

*Soma kisa hiki, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Zera na Atanasi wanasoma darasa la nne katika Shule ya Msingi Mbuyuni. Zera amejiwekea malengo katika masomo yake. Malengo hayo ni kufanya vizuri katika masomo yake hadi afike chuo kikuu. Amejiwekea ratiba ya kusoma na anaifuata. Pia hujifunza kwa bidii na kuwaomba walimu wamsaidie pale anapopata kikwazo. Katika muhula huu amekuwa wa kwanza darasani kimasomo. Kwa upande wa Atanasi, yeye hakujiwekea malengo yoyote. Hana ratiba yoyote ya kujisomea na hana bidii katika masomo. Hajui anataka kuwa nani baada ya masomo yake. Katika mtihani wa muhula amekuwa wa mwisho kimasomo darasani.

**Zoezi la 6**

1. Je, umejifunza nini kutoka kwa Zera?
2. Je, kujiwekea malengo kumemsaidiaje Zera?
3. Je, ungekuwa rafiki yake Atanasi ungemshauri nini?
4. Malengo gani umewahi kujiwekea katika maisha yako?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Andika mambo utakayofanya ili uweze kufanikiwa kimasomo kwa mpangilio ufuatao:

(a) Taja malengo yako.

(b) Eleza jinsi utakavyofanya kufikia malengo yako.

## Kutatua matatizo

Baada ya kujifunza jinsi ya kujiwekea malengo, sasa utajifunza jinsi ya kutatua matatizo yanayokukabili maishani.

Je, unapopata tatizo unachukua hatua gani? Je, tatizo likiwa nje ya uwezo wako utafanya nini?

*Soma mazungumzo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Tila:** Alama zangu kwenye Hisabati siyo nzuri. Sijui nifanyeje?

**Jema:** Si uachane na Hisabati uongeze juhudi kwenye masomo mengine?

**Tila:** Hili ni tatizo kwangu. Lazima nilitatue.

**Jema:** Mbona siku zote umeshindwa kulitatua?

**Tila:** Ni kweli, lakini itabidi niongeze bidii sasa.

**Jema:** Bidii gani hiyo?

**Tila:** Nitajiwekea ratiba ya kujisomea nyumbani na kuifuata. Nitafanya maswali kumi ya Hisabati kila siku.

**Jema:** Mimi Hisabati imenishinda. Wewe hangaika tu.

**Tila:** Mimi sikubali naamini bidii yangu itanisaidia.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Jema:** Mimi nasubiri matokeo tu!

**Tila:** Hili tatizo liko ndani ya uwezo wangu. Nitaongeza bidii zaidi na kutafuta msaada kwa mwalimu wa Hisabati.

**Jema:** Sawa rafiki yangu umefanya uamuzi mzuri. Ukifanikiwa nami nitaiga mbinu zako.

**Tila:** Nina hakika nitafanikiwa.

**Zoezi la 7**

1. Je, umejifunza nini kutokana na tabia ya Tila katika mazungumzo uliyosoma?
2. Je, ni matatizo gani uliyowahi kukabiliana nayo?
3. Ukipewa nafasi utamshauri nini Jema?

**Kazi ya kufanya**

Jadili na wenzako kuhusu namna ya kufaulu somo unalofanya vibaya. Andika maelezo hayo kwenye daftari lako.

FOR ONLINE USE ONLY

## Kupokea ushauri

Ili uweze kutekeleza malengo uliyojiwekea ni vyema kupokea ushauri mzuri kutoka kwa wengine.

Je, unafikiri unahitaji ushauri kwenye mambo gani? Ni watu gani wanaoweza kukupa ushauri huo? Je, kuna faida zipi za kupokea ushauri unaofaa?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Soma kisa hiki, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Paulo na Lusiana ni marafiki wanaosoma darasa la nne katika shule ya Msingi Jitegemee. Walipofika darasa la nne wazazi wa Paulo walikosa uwezo wa kumpa mahitaji ya shule. Paulo alikosa sare za shule, madaftari na vitabu. Pia, alifikiria kuacha shule na kutafuta kazi za nyumbani ili aweze kujipatia fedha. Alimshirikisha rafiki yake Lusiana kuhusu jambo hilo. Lusiana alimwambia, "Sikushauri uache shule rafiki yangu. Elimu ndio ufunguo wa maisha. Twende tukazungumze na mwalimu wa darasa kuhusu jambo hili." Paulo alikubali ushauri na walienda kwa mwalimu. Mwalimu wa darasa aliamua kumsaidia Paulo ili aweze kuendelea na masomo yake.

**Zoezi la 8**

1. Ni kwa nini Paulo aliomba ushauri?
2. Wewe ungekuwa Paulo ungefanya nini?
3. Je, ungekuwa wewe ni Lusiana ungemshauri nini Paulo?
4. Ni ushauri gani umeshawahi kupokea?
5. Taja faida ulizopata baada ya kupokea ushauri.

**Kazi ya kufanya**

Zungumza na mzazi au mlezi akueleze ushauri wowote aliowahi kupokea na jinsi ulivyomsaidia. Andika maelezo hayo nyuma ya daftari.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 9

1. Orodhesha matendo mawili yanayoashiria mtazamo chanya.
2. Orodhesha faida nne za kujifunza kwa makundi.
3. Andika faida tatu za kujitegemea.
4. Taja njia mbili zinazofaa kutumika kutatua tatizo la kushindwa katika masomo.

## Msamiati

| | |
|---|---|
| **Kutafakari** | kufikiria jambo kwa umakini |
| **Malengo** | mambo yanayotarajiwa |
| **Mtazamo chanya** | mawazo au msimamo mzuri alionao mtu kuhusu suala fulani |
| **Stadi** | maarifa ya kufanya jambo |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi

## Kujifunza mambo kiyakinifu

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza kujenga tabia ya kufahamu mambo mbalimbali kwa undani. Ili ufaulu vyema katika masomo yako, unapaswa kujifunza kwa undani mambo unayofundishwa. Unapojifunza masomo yako kwa kina utaweza kufaulu vyema na kuendelea na masomo ya juu. Umahiri utakaoupata katika sura hii utakuwezesha kutumia mbinu mbalimbali za kuchanganua mambo kwa usahihi. Pia, utakuwezesha kupata maarifa kutoka vyanzo tofauti na kuvihusianisha na uhalisia katika maisha ya kila siku.*

### Vyanzo vya taarifa mbalimbali

Ili uweze kufanikiwa katika jambo lolote ni muhimu kuwa na taarifa zinazohusu jambo hilo. Kwa mfano, ukitaka kuandaa shamba ni lazima upate taarifa za hali ya hewa. Vilevile, unapokuwa shuleni unaweza kupata taarifa za masomo yako kutoka vyanzo mbalimbali. Vyanzo hivyo vinajumuisha kusoma ubao wa matangazo, kuhudhuria paredi na baraza la kufungua au kufunga shule. Hivi ni baadhi ya vyanzo vya taarifa shuleni.

*Angalia picha zifuatazo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

1.




FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2.



3.



4.



**Kielelezo namba 1:** *Vyanzo mbalimbali vya taarifa*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 1**

1. Je, ni vyanzo gani vya taarifa vilivyopo kwenye picha?
2. Ni taarifa gani unazoweza kuzipata kwenye vyanzo hivi?
3. Je, ni vyanzo gani vingine vya taarifa unavyovifahamu?
4. Taarifa unazopata huwa unazifanyia nini?

**Kazi ya kufanya**

Chunguza na orodhesha vyanzo vya taarifa vinavyopatikana katika eneo unaloishi.

## Kujifunza kutokana na makosa ya watu wengine

Katika sehemu hii utajifunza kuhusu umuhimu wa kuchunguza makosa ya wengine ili kuyaepuka. Je, wewe huwa unajifunza nini kutokana na mafanikio ya watu wengine? Je, wewe huwa unajifunza nini kutokana na makosa ya watu wengine?

*Soma kisa hiki, Kisha jibu maswali yanayofuata.*

Kulwa ni mwanafunzi wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Kigwa. Anaye kaka aitwaye Amosi. Amosi hakufanikiwa kuhitimu elimumsingi, alifukuzwa shule akiwa darasa la sita. Hali hii ilitokana na kuhusishwa na biashara ya kuuza na kutumia dawa za kulevya. Siku moja, Kulwa akiwa njiani kutoka shuleni alikutana na vijana wawili wa kiume waendesha bodaboda. Vijana hao walianza kumrubuni ili aanze kuuza na kutumia dawa za kulevya. Kulwa hakukubali. Aliwaambia kwamba anafahamu hasara za kutumia dawa za kulevya

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kutokana na makosa ya kaka yake. Baadaye Kulwa alitoa taarifa za tukio hilo kwa wazazi wake na shuleni. Vilevile, aliwaasa wanafunzi wenzake darasani wasikubali kurubuniwa ili kujihusisha na uuzaji na utumiaji wa dawa za kulevya.

**Zoezi la 2**

1. Je, ni makosa gani yanayotajwa katika kisa hiki?
2. Je, Kulwa amejifunza nini kutoka kwa Amosi?
3. Umewahi kujifunza nini kutokana na makosa ya wenzako?

**Kazi ya kufanya**

Jadiliana na wazazi au walezi kuhusu makosa waliyowahi kuyafanya katika maisha yao. Andika habari fupi kueleza ulichojifunza kutokana na makosa yao.

## Kujenga hoja

Unapozungumzia jambo lolote unapaswa kutoa sababu sahihi zinazothibitisha ukweli wa jambo hilo. Kwa mfano, unapojibu maswali darasani, unapojadiliana na wenzako au kujitetea, unapaswa kuthibitisha usahihi wa majibu yako. Aidha, unapoomba kuhamishwa kutoka shule moja kwenda nyingine inakupasa kutoa sababu sahihi. Sababu hiyo itamshawishi mzazi au mlezi kukubali ombi lako. Kwa kutenda vitendo hivyo utakuwa unajenga hoja.

Je, umewahi kuwasilisha hoja yoyote kwa wenzako, walimu, wazazi au walezi?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Levina na Joshua ni watoto wa Mzee Heri. Wote wanasoma darasa la nne katika Shule ya Msingi Msufini. Levina alikuwa anafanya vibaya sana darasani. Kila somo alipata alama za chini. Joshua alikuwa anafanya vizuri sana darasani. Mwalimu wa darasa wa Levina alitaka kufuatilia sababu za watoto hawa kuwa tofauti kiasi hicho. Baada ya uchunguzi aligundua kuwa Levina hufanya shughuli nyingi za nyumbani. Hakuwa na muda wa kutosha kupumzika na kujisomea. Lakini Joshua hakuwa na shughuli yoyote. Alitumia muda mwingi kucheza, kupumzika na kujisomea. Pia, alikuwa na muda wa kwenda maktaba. Levina aliona kuwa hali yake inazidi kuwa mbaya kimasomo. Hivyo alienda kumweleza mwalimu wa darasa mambo yalivyo nyumbani kwao.

Mwalimu aliwaita wazazi wa Levina na Joshua pamoja na watoto wao. Yafuatayo ni majadiliano yao:

**Mwalimu:** Nimewaita hapa wazee ili tuongelee hali za watoto kimasomo. Joshua hana tatizo lolote, lakini Levina anafanya vibaya sana katika masomo. Kuna tatizo gani?

**Baba Joshua:** Joshua ni mwanaume lazima afanye vizuri. Wanawake si unajua ni dhaifu kwa kila jambo?

**Mwalimu:** Joshua, hebu nipe ratiba yako ya siku ukiwa nyumbani.

**Joshua:** Nikitoka shuleni huwa napewa chakula. Baada ya chakula napumzika kidogo halafu naenda kucheza mpira. Nikirudi nafanya kazi za shuleni

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

hadi muda wa chakula cha usiku. Nikimaliza kula ninaangalia kidogo runinga, ninaandaa sare za shule na kwenda kupumzika ifikapo saa tatu. Asubuhi huwa ninaamka saa 12 kuoga, kupata kifungua kinywa na hatimaye kujiandaa kwenda shuleni.

**Mwalimu**: Na wewe Levina elezea ratiba yako.

**Levina**: Mimi nikifika nyumbani, huwa ninahudumia kwanza mifugo. Baada ya hapo ninaanza kupika. Baada ya kupika, ninaandaa vitafunwa kwa ajili ya kifungua kinywa. Kisha, ninakula na kwenda kupumzika. Asubuhi huwa ninaamka saa 10 na kuanza kufanya usafi wa nyumba. Nikimaliza ninaosha vyombo na kufagia uwanja. Hatimaye, ninaandaa kifungua kinywa, ninakunywa chai na mwisho ninajiandaa kwenda shuleni.

**Mwalimu**: Huwa unapumzika saa ngapi Levina?

**Levina**: Saa sita usiku.

**Mwalimu**: Kwa nini Joshua hasaidiani na Levina kwenye kazi za nyumbani?

**Baba Joshua**: Hizo ni kazi za wanawake, atafanyaje mtoto wa kiume?

**Mwalimu**: Huoni kwamba binti yako anakosa muda wa kupumzika, na hata kufanya kazi zake alizopewa shuleni?

**Baba Joshua**: Kwani mila na desturi zinasemaje kuhusu mtoto wa kike?

**Mwalimu**: Mila na desturi zipo. Hata hivyo, mgawanyo wa kazi kwa watoto ni muhimu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Baba Joshua**: Kwani wewe unashaurije?

**Mwalimu**: Watoto wote hawa ni wa kwako. Hakuna ambaye ni bora kuliko mwingine. Lazima wanapofika nyumbani wafanye majukumu yao kwa usawa.

**Baba Joshua**: Asante mwalimu! Nitatekeleza yote tuliyo yazungumza kwa manufaa ya watoto wangu.

**Zoezi la 3**

Andika **ndiyo** kwa sentensi sahihi au **hapana** kwa sentensi isiyo sahihi.

1. Joshua alikuwa anafanya vizuri darasani kwa sababu alipata muda wa kupumzika na kufanya kazi za shuleni ________.
2. Levina alikuwa anafanya vibaya darasani kwa sababu alikuwa mzembe wa kusoma __________.
3. Hoja ya Levina na Joshua kuhusu usawa ilimfanya baba Joshua kukubali maelezo ya mwalimu __________.
4. Unapojadiliana na wenzako kwa kutoa sababu sahihi utakuwa umejenga hoja ___________.

Majadiliano uliyosoma yanakufundisha namna mwalimu alivyojenga hoja ili kubadilisha mtazamo wa baba Joshua. Unapojenga hoja unapaswa kutumia sababu madhubuti zinazoonesha kwamba maelezo yako ni sahihi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Onesha umuhimu wa elimu kwa watoto wa kike na wa kiume kwenye familia. Andika hoja hizo kwenye daftari lako.

**Zoezi la 4**

1. Je, ni njia zipi za upatikanaji wa habari unazozitumia?
2. Ni mambo gani uliyowahi kujifunza kutokana na makosa ya watu wengine?
3. Ni hasara zipi unazoweza kupata kwa kuamua jambo kabla ya kutambua athari zake?
4. Andika hoja tatu kueleza umuhimu wa elimu kwa watoto wa kike na wa kiume.

**Msamiati**

| | |
|---|---|
| **Hoja** | jambo lenye sababu za kina |
| **Kuhitimisha** | kufikia uamuzi wa mwisho |
| **Kujenga hoja** | kutoa mawazo yenye sababu sahihi |
| **Mwadilifu** | mtu anayeishi kwa kuzingatia miongozo ya jamii |
| **Rubuni** | eleza au fanya jambo lisilo la kweli ili kumshawishi mtu akubali jambo unalolitaka |
| **Yakinifu** | jambo lenye uhalisia, ukweli, uthibitisho au uhakika |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Moja

## Kuishi na watu wa asili tofauti

Darasa la tatu ulijifunza kuishi na watu wenye asili tofauti. Katika sura hii utajifunza kuheshimu tofauti za kiutamaduni, na kujenga urafiki mwema na watu wa mataifa mengine.

### Kuthamini lugha za asili

Katika jamii zetu kuna lugha mbalimbali za asili, Lugha hizo hutumiwa na jamii kuwasiliana. Lugha yako ya asili ni ipi?

*Soma salamu za makabila yanayofuata, kisha jibu maswali.*

**Kingoni**
Tukuwoni mawu

**Kihaya**
Marairota

**Kigogo**
Mbukwenyi yaya

**Kihehe**
Kamwene yuva

**Kisambaa**
Uinuke zeze mnaa

**Kisangu**
Ulamwishe mai

**Kielelezo namba 1:** *Kuthamini lugha za asili*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Je, umegundua nini kwenye michoro hiyo? Ni vyema ukatambua kuwa katika jamii yetu tunaishi na watu wa makabila tofauti. Kila kabila lina lugha yake ya asili na hutumia lugha hiyo kuwasiliana. Je, wewe huwa unawasiliana kwa kutumia lugha yenu ya asili?

*Soma kisa na mazungumzo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Siwatu ni mtoto wa mwisho katika familia ya Mzee Hoza. Wanaishi katika kijiji cha Bwama. Siwatu anasoma darasa la nne katika Shule ya Msingi Bwama. Wakati wa likizo, Siwatu humtembelea shangazi yake anayeishi kijiji cha Mtimbwani. Siku moja asubuhi akiwa kwa shangazi yake, alisikia mtu akibisha hodi, "Hodi nyumba hii". Siwatu alienda kufungua mlango. Alikuwa ni mzee Mgalla, mzee maarufu pale kijijini. Hata hivyo, Siwatu hakumfahamu. Yule Mzee alisema, "*Ukalamkaze*" Siwatu akabaki ameduwaa! Mzee Mgalla akagundua kuwa Siwatu ni mgeni katika kijiji kile. Akauliza, *"Mwenye nyumba hii nimemkuta?"* Siwatu akamjibu kuwa hayupo, ameenda mjini. Yule mzee akaondoka akaahidi kurudi baadaye. Shangazi yake aliporudi mazungumzo yalikuwa kama ifuatavyo:

**Siwatu:** Habari za mjini shangazi?

**Shangazi:** Nzuri mwanangu! Kwema hapa?

**Siwatu:** Kwema! Alikuja mgeni ila simfahamu kwa jina.

**Shangazi:** Sawa, amesemaje?

**Siwatu:** Atakuja tena jioni. Ila amezungumza lugha ambayo sikuielewa.

**Shangazi:** Amezungumza maneno gani hayo?



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Siwatu:** Amesema *"ukalamkaze",* hivi alimaanisha nini?

**Shangazi:** Alimaanisha, 'umeamkaje' hiyo ni salamu ya watu wa kabila la Kidigo.

**Siwatu:** Je, ningemjibuje?

**Shangazi:** Ungemjibu, *"Sijambo, simanya ue".* Yaani sijambo sijui wewe.

**Siwatu:** Mimi ningejuaje shangazi! Je, ni lugha gani nyingine inayozungumzwa katika kijiji hiki?

**Shangazi:** Lugha ya Kisambaa, kwani kuna Wasambaa pia katika kijiji hiki.

**Siwatu:** Salamu yao nao ikoje?

**Shangazi:** Asubuhi, utasalimia kwa kusema, "*Shikamoo shangazi, uinuke zeze*"? Yaani ukimaanisha shikamoo shangazi, umeamkaje?

**Siwatu:** Ninashukuru shangazi. Nitajitahidi kujifunza lugha za asili.

## Zoezi la 1

1. Je, ni tabia ipi iliyooneshwa na Siwatu kwenye habari hii?
2. Ni lugha zipi za asili alizojifunza Siwatu kutokana na habari hii?
3. Taja lugha nyingine tano za asili zilizoko Tanzania.
4. Unamshauri nini mtu asiyefahamu lugha yao ya asili?

## Kazi ya kufanya

Chunguza majirani katika eneo unaloishi ili kubaini lugha zao za asili. Andika kwenye daftari lako salamu wanazozitumia.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Shughuli zinazofanywa na watu wenye asili tofauti

Je, unafahamu shughuli za asili zinazofanywa na watu wa kabila lako? Shughuli za asili katika eneo hutegemea rasilimali zilizopo, hali ya hewa, na mila na desturi. Mfano, Wapare hushiriki zaidi katika shughuli za ufinyanzi wa vyungu. Hii inatokana na eneo wanaloishi kuzungukwa zaidi na udongo wa mfinyanzi. Wamakonde hushiriki katika shughuli za uchongaji wa vinyago. Hii inatokana na mazingira yao kuwa na miti mingi ya mpingo. Miti hiyo inafaa sana kwa uchongaji wa vinyago. Pia, Wakerewe hushiriki katika shughuli za uvuvi wa samaki. Wakerewe hujishughulisha na uvuvi kwa sababu wanaishi katika kisiwa cha ukerewe kilichopo ziwa Victoria. Vilevile, watu wa kabila la Wanyakyusa hujishughulisha na ususi wa mikeka, vikapu na nyungo.

*Angalia picha hizi, kisha jibu maswali yanayofuata.*

1.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2.



3.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. 

**Kielelezo namba 2:** *Shughuli zinazofanywa na watu wenye asili tofauti*

## Zoezi la 2

1. Taja shughuli unazoziona katika picha namba moja hadi nne.
2. Ni watu wa makabila gani hufanya shughuli zinazoonekana katika picha namba moja hadi nne?
3. Orodhesha makabila mengine unayoyafahamu yanayofanya shughuli sawa na zinazoonekana katika picha namba moja hadi nne.
4. Je, ni shughuli zipi za asili zinafanywa na watu wa kabila lako?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Bainisha makabila matano tofauti, kisha jaza jedwali linalofuata.

| Na. | Kabila | Mkoa | Shughuli |
|---|---|---|---|
| 1. | Mpare | Kilimanjaro | Ufinyanzi |
| 2. | | | |
| 3. | | | |
| 4. | | | |
| 5. | | | |
| 6. | | | |

## Kujifunza utamaduni wa makabila mbalimbali

Bila shaka unatambua kuwa tunaishi na watu wa makabila mbalimbali wenye utamaduni tofauti. Watu hao wanaishi kwa kuzingatia mila na desturi za makabila yao. Je, unafahamu utamaduni wa kabila lako?

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Malenga ni mwanafunzi wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Uhuru iliyoko mkoani Iringa. Siku moja, wakati wa somo la Uraia na Maadili, mwalimu aliwaambia wanafunzi waeleze utamaduni wa makabila yao. Malenga alisimama kwa furaha na kusimulia kuhusu utamaduni wa kabila la Wahehe. Alisema, "Kabila la Wahehe kwa asili linapatikana mkoani Iringa. Ni miongoni mwa makabila maarufu katika kuenzi mila na desturi zake. Kihehe ndiyo lugha ya asili ya Wahehe. Wahehe huthamini

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

sana utamaduni wao na hii huwapa sifa kubwa. Wanasifiwa kwa uvumilivu, ujasiri na uchapaji kazi. Mtu mvivu hudharauliwa na kuchekwa na jamii nzima.

Wahehe hujihusisha na kilimo cha mazao ya chakula. Baadhi ya mazao hayo ni mahindi, mtama, mihogo, alizeti, kunde, na maharage. Mazao mengine ni viazi vitamu, viazi mviringo, karanga na ulezi. Wahehe hualikana wakati wa kupalilia na kuvuna. Kitendo hicho cha kualikana katika kazi huitwa *Mugove.* Wakati wa mavuno, mtu anayesaidiwa kazi huandaa pombe, togwa na kande kwa ajili ya watu aliowaalika.

Vilevile, wanapokutana hushikana mkono wa kulia. Kisha kila mmoja huubusu mkono wa mwenzake kwa kupokezana zaidi ya mara mbili. Kitendo hicho huitwa *Kunonela* au *Kwinonela*.

Baadhi ya miiko ya Wahehe ni kumnyooshea kidole mtu kwa lengo la kumkemea. Wakiamini kuwa kufanya hivyo ni kumtakia mwenzako jambo baya.

Wahehe hucheza ngoma ya *kiduo*. Hufunga *njuga* miguuni huku wakicheza kwa kumzunguka mpiga ngoma. Ngoma huchezwa wakati wa tambiko na siku ya kugawa vyombo vya marehemu. Nyumba za asili za kabila hili ni za udongo. Paa la nyumba huezekwa kwa nyasi kavu. Nyingine hutupiwa udongo juu yake ili kuepuka kuungua. Kiongozi mkuu wa kabila la Wahehe ni *mtwa*. Utaratibu wa kupata viongozi katika kabila la Wahehe ni wa kurithi".

Baada ya maelezo ya Malenga, wanafunzi wote pamoja na mwalimu walimshangilia na kumpongeza. Walimpongeza

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kwa bidii yake ya kujifunza kuhusu utamaduni wa kabila lake. Mwalimu aliwaasa wanafunzi kujielimisha kuhusu tamaduni mbalimbali ili waweze kuishi vyema na watu wengine.

## Zoezi la 3

1. Je, umejifunza mambo gani yanayotambulisha utamaduni wa Wahehe?
2. Ni mambo gani yanayotambulisha utamaduni wa kabila lako?
3. Je, utamshauri nini rafiki yako asiyejua utamaduni wa kabila lake?
4. Taja faida nne za kujifunza juu ya tamaduni za makabila mbalimbali.

## Kazi ya kufanya

Jadiliana na watu wa makabila mawili tofauti katika eneo unaloishi, kisha jaza jedwali lifuatalo. Namba moja imejazwa kama mfano.

| Na. | Kabila | Mkoa | Kiongozi | Lugha ya asili | Ngoma ya asili | Shughuli za kiuchumi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Msambaa | Tanga | Zumbe | Kisambaa | Mdumange | Kilimo na biashara |
| 2. | | | | | | |
| 3. | | | | | | |
| 4. | | | | | | |
| 5. | | | | | | |
| 6. | | | | | | |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kuheshimu utamaduni wa watu wengine

Mwanafunzi, ulipokuwa darasa la tatu ulijifunza kuheshimu tofauti ya mavazi, lugha, vyakula na ngoma. Vilevile, makazi na kazi za makabila ya Kitanzania. Katika sehemu hii utajifunza kuheshimu mila na desturi za makabila mengine.

*Tafakari matendo yafuatayo:*

1. Mtu amechonga meno na kutoboa masikio.
2. Mzee anafanya tambiko ikiwa ni dua ya kuomba mvua.
3. Watu wanacheza ngoma kusherehekea harusi.
4. Vijana wa kiume wamejipanga wakifanyiwa tohara.

Je, matendo hayo, yanaashiria nini?

*Soma majadiliano haya, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Bahati:** Jana tulipata shida sana mtaani kwetu.

**Riziki:** Shida ya nini tena?

**Bahati:** Kulikuwa na ngoma ya mdundiko ikipigwa kwa jirani yetu.

**Riziki:** Aah kumbe! Sasa shida ilikuwa wapi?

**Bahati:** Ile ngoma siipendi kweli? Walitupigia kelele mchana kutwa.

**Riziki:** Sasa ulitaka wafanye nini wakati wanadumisha mila zao? Mbona nyie mwezi uliopita mlileta ngoma ya mganda kwenye harusi ya kaka yako?

**Bahati:** Mganda ngoma ya wastaarabu wewe!

**Riziki:** Siyo vizuri rafiki yangu kudharau ngoma za wenzio.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

1. Je, ni tabia gani iliyooneshwa na Bahati?
2. Ni tabia gani iliyooneshwa na Riziki?
3. Je, ni tabia ipi inafaa kuigwa? Kwa nini?

## Kazi ya kufanya

Chunguza matukio ya kiutamaduni yanayotokea kwenye eneo unaloishi. Andika habari fupi ya nusu ukurasa kueleza namna jamii inavyoheshimu matukio hayo.

## Kuheshimu itikadi na imani mbalimbali

Ni vyema utambue kuwa kila mtu ana imani na itikadi kwa dini, timu au chama anachokipenda. Unapaswa kuheshimu imani na itikadi ya kila mmoja. Kwenye jamii yetu kuna itikadi mbalimbali za kisiasa na kidini.

*Angalia picha za bendera za baadhi ya vyama vya siasa nchini, kisha jibu maswali yanayofuata.*




**Kielelezo namba 3:** *Bendera za vyama vya siasa*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 5**

1. Taja vyama vingine vya siasa unavyovijua vilivyopo Tanzania.
2. Taja faida tatu za kuwa na vyama vingi vya siasa Tanzania.
3. Je, watu wenye itikadi na imani tofauti wanaweza kuishi pamoja?

*Tafakari matendo yafuatayo:*

1. Siku ya Ijumaa masomo yamekatishwa ili kuwaruhusu wanafunzi kwenda kuabudu.
2. Wanafunzi wa imani tofauti wamehudhuria vipindi vya dini kwenye vyumba tofauti.
3. Wanafunzi wameruhusiwa kuvaa mavazi yanayoendana na imani zao.
4. Wanafunzi hawajaenda shuleni kutokana na sherehe ya sikukuu ya kidini.

Umejifunza nini kutokana na matendo haya? Bila shaka utakuwa umetambua umuhimu wa kuheshimu imani za watu wengine. Kwa kufanya hivyo utajenga mshikamano na upendo na wenzako wa dini tofauti. Pia, utadumisha amani katika jamii.

*Fuatilia mazungumzo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Josefati:** Leo ni siku ya Ijumaa. Huendi msikitini?

**Amina:** Aaah! Nilikuwa nimesahau. Nashukuru kwa kunikumbusha. Ngoja nijiandae. Si unajua kipindi

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kinachofuata ni cha dini. Wewe pia unapaswa kuhudhuria.

**Josefati:** Mimi huwa ni mvivu wa kuhudhuria kipindi cha dini.

**Amina:** Siyo vizuri kukosa kipindi cha dini. Kwenye vipindi vya dini ndio tunapata mafundisho ya kujenga imani zetu.

**Josefati:** Nashukuru kwa ushauri wako Amina. Kuanzia leo nitahudhuria vipindi vyote vya dini.

**Amina:** Shule yetu ina utaratibu mzuri wa kuwaruhusu wanafunzi kuabudu. Tena kila mmoja huabudu kwa dini yake.

**Josefati:** Ni kweli kuheshimu imani za watu wote ni jambo la hekima.

**Amina:** Ndiyo hata kuwaruhusu wanafunzi kuvaa mavazi yanayoendana na imani zao ni ujasiri.

**Josefati:** Naipenda sana nchi yetu. Inaheshimu imani ya kila mmoja wetu.

**Zoezi la 6**

1. Ni matendo gani yanayoonesha kuheshimu imani ya mwigine?
2. Je, matendo kama hayo yana faida gani shuleni?
3. Ni matendo gani mengine ya kuheshimu itikadi na imani mbalimbali unayoyafahamu?

**Kazi ya kufanya**

Jadiliana na viongozi wa dini kuhusu faida za kuheshimu itikadi za watu wengine. Andika kwenye daftari lako faida mlizojadili.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Uhusiano mzuri na watu wengine

Sote tunaishi katika jamii yenye watu wenye tabia na sifa mbalimbali. Ili tuishi kwa amani, inatupasa kuwa na uhusiano mzuri na wengine.

*Angalia picha zifuatazo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

1. 


FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2.



3.



**Kielelezo namba 4:** *Matendo ya uhusiano mzuri na watu wengine*

Umejifunza nini katika picha hizo? Ni njia gani unazotumia ili kudumisha uhusiano mzuri na wenzako shuleni kwenu? Unawasaidiaje rafiki zako ili nao wawe na uhusiano mzuri

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

darasani kwenu? Kujenga uhusiano mzuri na watu wengine ni jambo zuri maishani mwetu. Zipo njia mbalimbali zinazoweza kukusaidia kujenga uhusiano mwema na wenzako. *Je, unazifahamu njia hizo?*

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Regina ni msichana anayesoma darasa la nne katika Shule ya Msingi Kiloleni. Yeye ni kiranja wa darasa la nne. Hupenda kudadisi matatizo waliyonayo wanafunzi wenzake na kuripoti kwa mwalimu wa darasa. Huripoti matatizo kama ugomvi kati ya wanafunzi, na hujaribu kuyatatua akishirikiana na walimu. Darasa lao lina furaha na amani kwa sababu ya uongozi wake.

Siku moja Ali na Sheila walitaka kupigana darasani. Regina aliwaona na kuwazuia. Aliwaambia kuwa ugomvi na kupigana huleta chuki na kuondoa upendo. Aliwaambia wanafunzi wengine kuwa haifai kuchokozana. Regina aliwasisitiza wenzake kuwa ili wafaulu inabidi wapendane. Wanafunzi wote walifurahi. Sasa Ali na Sheila ni marafiki. Wao husoma na kucheza pamoja. Pia, matokeo yao katika mitihani ni mazuri.

**Zoezi la 7**

1. Umejifunza nini kutokana na habari uliyosoma?
2. Ni kwa namna gani Regina hujenga uhusiano mzuri na wenzake?
3. Je, wewe unajengaje uhusiano mzuri na wenzako katika darasa lako?
4. Utafanya nini ili kuwasaidia rafiki zako kuwa na uhusiano mzuri?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 8

*Chagua herufi yenye jibu sahihi, kisha andika maneno yake kwenye nafasi zilizoachwa wazi.*

1. _______, ________ na _______ ni baadhi ya makabila yaliyotajwa kwenye sura hii.
   (a) Wangoni, Waha na Wagogo
   (b) Wahehe, Wasambaa na Wagogo
   (c) Wahaya, Wangoni na Wanyamwezi
   (d) Wamwela, Wasangu na Wahehe

2. Kuheshimu utamaduni wa watu wengine huleta ________.
   (a) Upendo na mshikamano
   (b) Ujasiri na upendo
   (c) Mshikamano na upole
   (d) Kelele na utulivu

3. Shughuli mbili za asili zilizotajwa katika sura hii ni_______.
   (a) Uchongaji na kilimo cha pamba
   (b) Ufinyanzi wa vyungu na uchongaji
   (c) Uvuvi wa samaki na kurina asali
   (d) Kurina asali na uchongaji

4. Faida za kuhusiana vyema na wenzako shuleni ni pamoja na _____________.
   (a) Kuleta chuki
   (b) Kuondoa upendo
   (c) Kufaulu vizuri katika mitihani
   (d) Kutokushirikiana

FOR ONLINE USE ONLY

## Kazi ya kufanya

Jadiliana na ndugu zako wakueleze njia walizotumia kujenga uhusiano mzuri na watu wengine. Andika kwenye daftari lako njia ambazo ni tofauti na unazozitumia.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine

Kuna faida nyingi za kushirikiana na watu wa mataifa mengine. Watanzania huweza kufaidika kibiashara, elimu na michezo. Je, unayafahamu mataifa mengine zaidi ya Tanzania? Je, Tanzania inashirikiana vipi na mataifa hayo?

*Soma ramani ifuatayo:*




**Kielelezo namba 5:** *Mataifa yanayounda Afrika Mashariki.*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Je, umegundua nini katika ramani hiyo? Je, unawafahamu marais wanaoongoza nchi hizo?

## Kuboresha uhusiano na mataifa mengine

Ziko mbinu kadhaa za kujenga uhusiano bora kati ya Tanzania na mataifa mengine.

Ni kwa namna gani Tanzania inajenga uhusiano na mataifa mengine?

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Tanzania hushirikiana na mataifa mengine katika mambo mbalimbali. Tanzania ni mwanachama wa jumuiya mbalimbali za kimataifa. Kwa mfano, Tanzania ni nchi mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nchi nyingine katika jumuiya hiyo ni Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda na Sudan Kusini.

Kiutamaduni, Tanzania hushirikiana na mataifa mengine katika michezo, muziki, na filamu. Tumekuwa tukishiriki mashindano mbalimbali ya michezo yanayohusisha mataifa mengine kama Kenya na Uganda. Vilevile, watanzania hujifunza lugha na utamaduni wa mataifa mbalimbali. Kwa mfano, watanzania hujifunza Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kikorea, Kijapani, Kirusi na hata Kichina. Kupitia lugha hizi Watanzania huweza kuwasiliana na watu wa mataifa mengine. Hujifunza utamaduni wao, siasa na hata uchumi wao. Watu wa mataifa mengine pia hujifunza Kiswahili ili waweze kuifahamu Nchi yetu na watu wake.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Pamoja na hayo, Tanzania hushirikiana na mataifa mengine kwa kuuza bidhaa zake. Mfano wa bidhaa hizo ni mazao ya biashara kama pamba na kahawa. Bidhaa nyingine ni madini na samaki. Pia hununua bidhaa kama nguo, mashine mbalimbali, na vyombo vya usafiri. Vilevile, watu wa mataifa mengine huja kuwekeza katika Nchi yetu.

Yatupasa kuonesha ukarimu kwa watu wa mataifa mengine wanapotembelea Tanzania. Tunaweza kufanya hivyo kwa kuwaelekeza jinsi ya kupata huduma wanazotaka. Mfano, pale wanapotaka kutembelea mbuga za wanyama na vivutio vingine vya utalii. Tunaweza kuwapa elimu kuhusu jamii ya watanzania kama vile utamaduni wetu. Vilevile, tuwalinde dhidi ya hatari mbalimbali. Mfano, tunaweza kuwaelekeza maeneo salama ya kufikia, usafiri salama na muda mzuri wa kutembea.

**Zoezi la 9**

1. Je, ni kwa namna gani Tanzania hujenga uhusiano na mataifa mengine?
2. Ni tabia gani za Watanzania zinazopendwa na watu wa mataifa mengine?
3. Taja nchi mbili ambazo ungependa kuzitembelea.

FOR ONLINE USE ONLY

**Kazi ya kufanya**

Jadiliana na wenzako aina ya bidhaa za Tanzania zinazouzwa nje ya Nchi. Orodhesha bidhaa hizo katika daftari lako.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Urafiki mwema baina ya Tanzania na mataifa mengine

Hadi sasa umejifunza namna Tanzania inavyoboresha uhusiano na mataifa mengine. Je, unaijua misingi ya urafiki baina ya Tanzania na mataifa mengine?

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Tanzania ni nchi inayosifika kwa kuwa imejenga urafiki na mataifa mengi. Urafiki huo umetokana na matendo mazuri ambayo Watanzania hufanya kwa watu wa mataifa hayo. Watanzania walijitolea uhai wao, hali na mali kuyakomboa mataifa mengine ya Afrika. Mataifa hayo ni kama vile Msumbiji, Angola na Afrika ya Kusini. Pia, Tanzania inashiriki kutatua migogoro ya mataifa mengine. Baadhi ya mataifa hayo ni Rwanda, Burundi na Somalia. Hata hivyo, migogoro hiyo inapotokea watu hukosa amani na kukimbia huku na kule. *Je, umeshawahi kusikia neno wakimbizi?* Migogoro husababisha watu kukimbia nchi zao na kuhamia nchi jirani. Watu hao huitwa wakimbizi. Tanzania imekuwa ikipokea wakimbizi kutoka nchi za jirani na kuwahifadhi kwenye kambi. Kwa mfano, zipo kambi za wakimbizi mkoani Kigoma, Kagera na Katavi.

Jambo jingine ni ushirikiano katika matumizi ya miundo mbinu. Ipo miundo mbinu inayotumiwa na Nchi yetu pamoja na nchi nyingine kwa mfano; bandari na reli. Baadhi ya mataifa hutumia bandari za Tanzania kupitisha mizigo yao. Mataifa hayo ni kama vile Malawi, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Rwanda na Uganda. Reli ya uhuru (TAZARA) ni kielelezo cha uhusiano mwema baina ya Tanzania na

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Zambia. Pia, kujengwa kwa bomba la mafuta kutoka Uganda hadi Tanzania kunaimarisha uhusiano baina ya Tanzania na Uganda.

Vilevile, kuwepo kwa rasilimali mbalimbali Tanzania huwavutia watu wa mataifa mengine kuja kuwekeza na kutalii. Baadhi ya rasilimali hizo ni madini, misitu, milima na mbuga za wanyama. Uhusiano huu pia huimarishwa na tunu za amani na utulivu.

**Zoezi la 10**

1. Ni mambo gani yanajenga urafiki mwema baina ya Tanzania na mataifa mengine?
2. Je, kuna faida gani za kuwa na uhusiano bora na mataifa mengine?

**Kazi ya kufanya**

Fanya uchunguzi wa taarifa unazozisikia kwenye redio na runinga. Pia, unazozisoma katika magazeti kuhusu uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine. Andika habari fupi kueleza ulichokibaini katika taarifa hizo.

## Utandawazi

Katika nyakati za sasa watu huwasiliana, husambaza bidhaa na kusafiri kwa urahisi. Hii inatokana na ubora wa vifaa vya mawasiliano kama simu na kompyuta.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Tafakari matendo yafuatayo:*

1. Vijana wanaangalia mpira kwenye runinga huku wakishangilia.
2. Mwalimu anahadithia wenzake tukio lililotokea katika nchi ya jirani.
3. Watoto wanaangalia tamthiliya kwenye runinga.
4. Mtoto anaiga mavazi yasiyofaa aliyoyaona kwenye runinga.
5. Mwanafunzi anatumia kompyuta kuandika taarifa.

Je, umegundua nini? Unajifunza nini kutokana na matendo haya?

*Soma mazungumzo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Bwana Kazimoto ni mwalimu wa Uraia na Maadili darasa la nne. Siku moja alikuwa anafundisha kuhusu utandawazi. Hebu fuatilia majadiliano yake na wanafunzi.

**Mwalimu:** Leo tutajifunza kuhusu utandawazi. Je, mmewahi kusikia neno utandawazi?

**Juhudi:** Mwalimu hilo ni jambo jipya kabisa.

**Mwalimu:** Je, tunapataje habari za matukio yanayotokea nchini mwetu?

**Salome:** Mwalimu tunapata habari kupitia redio na runinga.

**Mwalimu:** Umejibu vizuri. Je, ni vitu gani vingine vinatupa habari?

**Sikujua:** Ni simu, vitabu, magazeti na kompyuta.

**Mwalimu:** Ni taarifa gani nyingine mnazipata kutokana na vyombo hivyo?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Juhudi:** Mimi huwa naangalia mashindano ya mpira wa miguu, filamu, na muziki.

**Mwalimu:** Upatikanaji wa taarifa kutoka sehemu tofauti ni sehemu ya utandawazi. Utandawazi umefanya dunia imekuwa kama kijiji.

**Salome:** Mwalimu, unamaanisha nini kusema dunia imekuwa kama kijiji?

**Mwalimu:** Taarifa nyingi huenda kwa kasi sana. Mfano, Rais wetu akiwa anahutubia Taifa, taarifa hiyo huweza kuonekana dunia nzima muda huohuo. Taarifa huenea kwa haraka zaidi. Hii ni kutokana na maendeleo ya teknolojia ya mawasiliano.

**Juhudi:** Ahaa! Ndiyo sababu bibi yetu aliyeko kijijini alipata taarifa za uchaguzi wa Marekani kwa njia ya runinga.

## Zoezi la 11

1. Je, ni faida gani tunapata kutokana na utandawazi?
2. Ni madhara gani tutapata ikiwa hatutatumia utandawazi vizuri?
3. Utafanya nini kumsaidia rafiki yako asiyeelewa kuhusu faida za utandawazi?

## Kazi ya kufanya

Zungumza na wazazi au walezi kuhusu faida na hasara za utandawazi. Andika taarifa hiyo kwenye daftari lako.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Msamiati

| | |
|---|---|
| **Imani** | hali ya kukubali kuwa kitu fulani kipo au ni kweli |
| **Itikadi** | msimamo wa mtu au watu kuhusu jambo fulani |
| **Kambi** | makazi ya muda |
| **Tambiko** | ibada ya kiasili ya kuabudu mizimu |
| **Utandawazi** | mfumo wa mawasiliano rahisi unaoziwezesha nchi nyingi duniani kuwasiliana na kushirikiana katika masuala ya biashara, siasa na teknolojia kwa njia ya mtandao uliounganishwa kwenye kompyuta, aipadi au simu |

FOR ONLINE USE ONLY

Vitabu vingine kutoka
Taasisi ya Elimu Tanzania

## Darasa la Nne



















ISBN 978-9987-09-324-3

*Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi*

Uraia na Maadili    Kitabu cha Mwanafunzi    Darasa la Nne